# MATATIZO YA MWANAMKE KATIKA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA *NYUSO ZA MWANAMKE*.

**NA**

**MONICA C RUTO**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

________________________ ____________________

**MONICA C. RUTO** **Tarehe**

Mtahiniwa

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo kikuu cha Nairobi.

________________________ ____________________

**Dkt. EVANS MBUTHIA** **Tarehe**

________________________ ____________________

**Bw . LEONARD SANJA** **Tarehe**

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu Joseph na Christine Maritim kwa kunilea na kunisomesha. Mungu azidi kuwaongezea miaka mingi duniani.

# SHUKRANI

Ninatoa shukrani maalum kwa wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Bw.Leonard Sanja kwa mawaidha yao mufti ambayo yalichangia katika ufanisi wa kazi hii.

Pia nawashukuru wanangu Nicholas, Victor, Ian na Alvine kwa kuvumilia kutengana na mama yao kwa sababu ya mradi huu . Mwisho ni kwa wale wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha mradi huu.

**IKISIRI**

Kazi hii inashughulikia matatizo yanayomkabili mwanamke katika *Nyuso za Mwanamke (*2010) ya Said A Mohammed na *Kidagaa Kimemwozea* (2012) ya Ken Walibora na athari zake kwa jamii .Tuliangalia matatizo ya wanawake na athari zinazotokana na matatizo hayo.

Pia tumeangazia mitazamo ya waandishi kuhusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike . Sababu za kuchagua mada pia zimeelezwa. Yaliyoandikwa kuhusu mada hii ni mengi kama tutakavyoona hapo baadaye.

Misingi ya Nadharia ya Ufeministi na mihimili yake ndiyo iliyoongoza utafiti wetu. Nadharia hii ya Ufeministi ni kwa mujibu wa wahakiki kama Birke (1986), Luvenduski, Randall (1993 ) na wengineo.

Nadharia ya Ufeministi inatumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo kama mojawapo wa mihimili yake muhimu . Mbinu ya kusoma maktabani ilitumika, ambapo tulirejelea makala mbalimbali yakiwemo majarida, tasnifu na vitabu kwa lengo la kupambanua suala la utafiti na nadharia kwa kina.

YALIYOMO UKURASA

Ungamo ..................... ii

Tabaruku ..................... iii

Shukrani ..................... iv

Ikisiri ..................... v

Yaliyomo ..................... vi

SURA YA KWANZA ..................... .1

1.0 Utangulizi ..................... 1

1.1 Suala la utafiti ..................... 1

1.2 Madhumuni ya utafiti ..................... 2

1.3 Maswali ya utafiti ..................... 3

1.4 Sababu za kuchagua mada. ..................... 3

1.5 Upeo na mipaka ..................... 4

1.6. Msingi wa kinadharia. ..................... 5

1.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ..................... 8

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada. ..................... 9

1.8 Njia za utafiti ..................... 12

SURA YA PILI: MATATIZO YA WANAWAKE KATIKA *KIDAGAA KIMEMWOZEA NA NYUSO ZA MWANAMKE*. ..................... 14

2.0 Utangulizi ..................... 14

2.1 Ndoa ya lazima. ..................... 15

2.2 Kudharauliwa......19
2.3 Dhuluma za kimapenzi......22
2.4 Lugha kama chombo cha kudhulumu......25
2.5 Kutawishwa......27
2.6 Kunyimwa haki za kuchuma mali na kurithi......30
2.7 Kukanwa na jamii......33
2.8 Hitimisho......35
**SURA YA TATU: ATHARI MBALIMBALI ZINAZOTOKANA NA MATATIZO YA WANAWAKE**......38
3.0 Utangulizi......38
3.1 Kusambaratika kwa ndoa......39
3.2 Mauti......44
3.3 Kukata tamaa kwa wanawake......46
3.4 Uhusiano wa unyumba......50
3.5 Upweke......51
3.6 Woga......53
3.7 Hitimisho......55
**SURA YA NNE: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**......57
4.0 Utangulizi......57
4.1 Matokeo......57
4.1.1 Mapendekezo......61
**MAREJELEO**......62

# SURA YA KWANZA.

## 1.0 Utangulizi

Tasnifu hii inashughulikia nafasi ya mwanamke katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ya Said A. Mohammed na *Kidagaa Kimemwozea* (2012) ya Ken Walibora. Kupitia utafiti wetu tumegundua kuwa mwanamke ameendelea kudhulumiwa kwa njia mbalimbali katika jamii. Mhusika wa kike amechukuliwa kama kiumbe duni na asiyestahili kuheshimiwa na kupewa hadhi na jamii. Tunaelezea jinsi mwanamke anavyochorwa katika jamii na pia kutoa picha kamili ya namna anavyotazamwa na wanaume kindoa , kisiasa, kidini na kiuchumi. Mwanamke hapewi nafasi ya kuchuma mali wala kurithi , kijieleza katika ndoa na hata kisiasa.

Katika riwaya hizi, inadhihirika kuwa mwanamke yuko chini ya mwanaume. Mwanamke hapaswi kupinga au kudadisi anayotenda mwanaume. Kupitia katika riwaya hizi, wahusika wa kike wameonyeshwa kupigania haki zao kama kuozwa kwa lazima, kutopewa nafasi ya kurithi mali na hata kupewa uhuru wa kujieleza. Hata hivyo wanakumbana na matatizo mengi wanapong’anga’nia kujinasua katika minyororo ya udhalimu.

Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Nyuso za Mwanamke,* matatizo mengi yanayowakumba wanawake yanadhihirika.Matatizo hayo ni kama vile, kupigwa, kuozwa kwa lazima, kimnya cha kulazimishwa, ukeketwaji, kubakwa na mengineo.

Matatizo hayo yanayowakumba wanawake hayajitokezi tu bali pia yanaathari kama vile, vifo, kusambaratika kwa ndoa, kukata tamaa, upweke , woga na mengineo.

## 1.1 Suala la utafiti

Kihistoria, wanawake wamekuwa wakichukuliwa kama viumbe duni na wasiokamilika. Higgs, C ( 2002 ), akimnukuu Olive Senior anasema, "Wanawake weusi wamekuwa waking'ang'ana dhidi ya mfumo chukulizi wa kijenda unaowatengea wanawake majukumu duni". Hata hivyo, wanaufeministi na wanafasihi tofauti wamekuwa wakitetea haki za wanawake kama Higgs (2002) anavyosema kuwa, "kwa zaidi ya miongo miwili, mengi yamefanywa kurudisha wanawake katika historia sio tu kama wahasiriwa wa kutobahatika na unyanyasaji bali pia kama watendaji na wavumbuzi mambo".

Mwanamke amekumbwa na matatizo mengi sana kutokana na udhalimu unaosababishwa na jamii yake. Tatizo tunalolishughulikia katika tasnifu hii ni matatizo yanayowakabili wanawake katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) *na Kidagaa`Kimemwozea* (2012) . Tumeweka bayana aina mbalimbali za matatizo anayokumbana nayo mwanamke. Aidha tumeangazia athari ambazo mwanamke anakumbana nazo kutokana na matatizo hayo kama zinavyodhihirishwa na watunzi. Vilevile mitazamo ya waandishi kuhusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike imewekwa wazi.

## 1.2 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo:

*i.* Kubainisha matatizo anayokumbana nayo mwanamke katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke (2010)* na *Kidagaa Kimemwozea (2012)* .

ii. Kubainisha athari zinazotokana na kuwa mwanamke kama zinavyojitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke na Kidagaa Kimemwozea*.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Je, matatizo yanayowakabili wanawake yamebainishwa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Kidagaa Kimemwozea* (2012)? .

ii. Kuna athari gani za kuwa mwanamke katika jamii kwa mujibu wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Nyuso* za *Mwanamke* ?.

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Kazi hii inadhamiria kuchangia katika kutambulisha mwanamke anavyodhalilishwa kwa kusudi la kutoa mwanga zaidi kuhusu jambo hili. Suala la utafiti lililomchochea mtafiti wa kazi hii ni matatizo anayokumbana nayo mwanamke katika jamii. Japo suala hili la udhalimu limeangaziwa na wengi kwa njia mbalimbali,utafiti wetu umeshughulikia mada hii kwa kushughulikia matatizo yanayowakabili wanawake na athari mbalimbali zinazotokana na matatizo hayo kama inavyodhibitishwa na watunzi. Tumeteuwa riwaya hizi kwa sababu zinaangazia suala la matatizo yanayowakumba wahusika wa kike katika viwango mbalimbali. Usawiri huu wa mwanamke umetuwezesha kuangazia changamoto anazokabiliana nazo katika jamii na mikakati anayoweza kutumia kuweza kujikomboa kutokana na matatizo hayo. Suala hili la udhalimu ndilo lililomchochea mtafiti wa kazi hii kushughulikia mada hii ya udhalimu kwa wahusika wa kike.

Aidha sababu ya kuchagua mada hii ni kuwa kulinganana na utafiti wetu tumegundua kuwa wahakiki wa hapo awali hawajamulika suala la unyanyasaji kwa wahusika wa kike katika riwaya hizi . Uhakiki wa hapo awali wa riwaya hizi ulizingatia wahusika kwa jumla na pia matumizi ya lugha. Kwa sababu hiyo tumekusudia kuangalia matatizo yanayowakumba wanawake na athari zinazotokana na matatizo hayo. Wanyonyi (2011) alishughulikia uhakiki wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamk*e iliyosheheni kimsuko, kimtindo na kisimulizi. Rono (2013) alishughulikia uhakiki wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, kwa kumulika maudhui na fani. Hii ni kazi iliyosheheni maudhui kwa ujumla lakini sisi tumeshughulikia suala la mhusika wa kike pekee katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Nyuso za Mwanamke* ambapo wahusika wa kike wanashughulikiwa katika riwaya hizo.

### 1.5 Upeo na mipaka

Utafiti huu umeangazia matatizo anayokumbana nayo mwanamke kama inavyojitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Tumeonyesha matatizo yanayomkabili mwanawake katika jamii na jinsi anavyojaribu kujikomboa kutokana na matatizo hayo.

Utafiti huu ulinuia kubainisha, kuainisha na kueleza jinsi unyanyasaji unaofanyiwa mwanamke ulivyojitokeza kupitia riwaya ya *Nyuso za Mwanamke na Kidagaa Kimemwoz*ea unavyodhihirika.

### 1.6 Msingi wa kinadharia

Nadharia iliyotumiwa katika kazi hii ni ya Ufeministi. Ufeministi ni dhana ambayo hujumlisha mikabala mbalimbali ya kiuhakiki ambayo licha ya tofauti zake inaelekea kukubaliana au kuafikiana kwenye masuala kadha na malengo yake ya kimsingi. Kimsingi, hii ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa na wahakiki wa ufeministi kama Birke (1986) na Lovenduski (1993) . Nia ni kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, dini, siasa, kijamii na kiuchumi. Pingu hizi zimejengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume.

Kwa mujibu wa Wafula R. na Njogu K. (2007), wanasema kuwa kulingana na wahakiki wa Kifeministi kama Birke (1986) , Lovenduski na Randal (1993), Ufeminsti ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao . Kinadharia, masuala ya Kifeministi yalianza kuzungumziwa karne ya kumi na tisa na kuanza kutia fora katika miaka ya sitini na ya sabini ya karne iliyopita ambapo wanawake hasa wa Kimagharibi walianza kuzungumza juu ya matatizo yao kwa nia ya kutafuta suluhisho.

Baadhi ya waasisi wa Nadharia hii ni Ramazanoghu, Millet , Mecham, miongoni mwa wengine. Ramazanoghu C. (1989) katika kitabu chake cha *Feminism and the Contraditions of the Oppression,* anasema kuwa masuala ya udhalimu dhidi ya mwanamke yalianza kuzungumziwa kuanzia miaka ya sitini na sabini;ambapo ilianza na wanawake hasa wa Kimagharibi. Wanawake hao walianza kuzungumza juu ya matatizo yao kwa utaratibu yaani katika machapisho . Wao walieleza kuwa

wanaume huwakandamiza wanawake na kwa jumla waume hufaidi kutokana na dhuluma hii. Mary Wollstonecraft (1972) ndiye anayefahamika kuwa mtaalamu wa kwanza kuyazungumzia masuala ya wanawake kwa utaratibu maalum. Miongoni mwa kazi nyingi zilizoandikwa na kuchapishwa na zilizochangia pakubwa zaidi katika maendeleo ya uhakiki wa Kifeministi lilikuwa *The Second Sex (1952*) lililoandikwa na Simone De Beauvoir. Lengo kuu la De Beauvoir katika kitabu hiki ni kubainisha, kukosoa na kuzipiga vita asasi zilizomdhalilisha na kumdunisha mwanamke. Germane Greer katika kitabu cha *The Female Eunuch* (1971) aliwahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa iliwafanya kumilikiwa na kukosa ubinafsi na uhuru wao. Nadharia ya Ufeministi, kulingana na Eselle B . Freedman (2002:3), ilianza Ufaransa na kutiliwa nguvu miaka ya sitini na kushika kasi miaka ya themanini na tisini na ikawa imesambaa ulimwengu mzima.

Kuna aina mbili kuu za Ufeministi kulingana na Bressler (2003: 150-151) na Christopher Miller (1990:255-256) . Ufeministi wa Kiafrika na Ufeministi wa Kimagharibi. Ufeministi tutakaotumia ni ule wa Kiafrika , kwa vile unaafiki mazingira ya Kiafrika ambayo riwaya tunazozishughulikia zinaanngazia. Ule wa Kimagharibi una matawi yanayoshirikisha ya Kifaransa, Kimerikani, Kiingereza miongoni mwa mengine.

Kimsingi , Ufeministi wa Kiafrika unajishughulisha na uhalisia wa maisha ya mwanamke katika miktadha ya kijamii , kitamaduni na kiuchumi. Unajishughulisha pia na haja ya kutaka kuonyesha jinsi miktadha hii inavyochangia kumnyanyasa, kumdunisha na kumdhalilisha mwanamke wa Kiafrika. Wanawake wa Kiafrika

wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni, ukeketaji wa wanawake, kutopewa nafasi ya kujieleza kuhusu masuala ambayo yanamhusu , desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa.

Njogu, K na R, Chimera (1999) katika *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu* , wanazungumzia Nadharia ya Ufeministi inayomtazama mwanamke. Wanapinga vile wanawake wamepuuzwa kwa sababu ya mifumo ya kijamii.Kazi yao inaoana na utafiti wetu kwani ina msukumo mkubwa kwa ukombozi wa wanawake.

Mbatia, M . (2002) anaeleza Ufeministi kuwa nadharia ya kifasihi ambayo kazi yake kuu ni kutetea haki za wanawake dhidi ya ukandamizaji katika jamii iliyo na mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Hii ina manufaa muhimu katika utafiti wetu .Inapigania usawa miongoni mwa wanadamu.

Wamitilila, K.W (2003) alieleza kuwa nadharia ya Kifeministi iliwekewa msingi wake na msukumo wa nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamanduni, kidini, kijamii kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii inadadisi msimamo na itikadi za kiume ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu zinazoshabiki ubabedume. Kwa kijumla watunzi wanaozungumza kuhusu masuala ya wanawake wamewatetea maslahi ya wanawake.Wamepigania usawa kati ya mume na mke katika asasi mbalimbali za maisha.

Ufeministi wa Kiafrika ndio utakaozingatiwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu riwaya tunazoshughulikia zimejikita katika mazingira ya Afrika, kwa hivyo itafaa

katika kazi yetu. Mwasisi wa Ufeministi wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981). Steady alieleza kwamba Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika, unatarijiwa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazochangia unyanyasaji wa wanawake wa Kiafrika. Steady alidai kwamba , " Ufeministi wa kweli ni ile hali ya kujinyima ulinzi wa kiume na jitihada za kuwa na busara na uwezo wa kujitegemea". Kulingana na Steady (1981: 30-37 ), Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ina sifa zifuatazo :

i. Inatambua uhusiano wake na Ufeministi wa Kimataifa lakini inafafanua Ufeministi ambao una mahitaji na malengo maalum yanayotokana na uhalisi wa maisha ya wanawake wa Kiafrika.

ii. Inatambua kihistoria kuwa katika jamii za Kiafrika kabla ya ukoloni , kulikuwa na watawala na mashujaa wanawake .

iii. Inaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na kupuuza unyanyasaji wa utumwa unaomkabili .

iv. Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na vita vya ukombozi wa kitaifa na ujenzi mpya wa jamii .

Kutokana na ufafanuzi haya , Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatetea haki na usawa wa wanawake dhidi ya udhalimu wa kijamii .

### 1.6.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

i. Nadharia hii inanuia kuwasawasisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za binadamu.

ii. Mtazamo huu pia unajaribu kuhamasisha wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.

iii. Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

iv. Pia nadharia hii hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Martin, A. (1975) katika kitabu chake cha, *Women and Imperialism* alisema kwamba wanamageuzi wa kike kule Kanada walichanganua kwa utaratibu vile wanawake waliathiriwa na utendakazi wa kibepari ulimwenguni kuanzia karne ya kumi na tisa hadi sasa. Kazi yake inatofautiana na kazi yetu kwa kiwango ambacho wanawake wanaathiriwa. Pia maeneo yao ni tofauti na maeneo ya utafiti wetu , yaani utafiti wetu ni wa Afrika ilhali maeneo ya Martin ni Kanada. Mawazo yake hata hivyo yanatusaidia kutoa mwanga kwa mwanamke wa Kiafrika kwani tunaamini kuwa mwanamke ana uwezo wa kujikomboa.

Kathleen, N. (1979) katika kitabu chake cha, *The Sisterhood of Man,* alisema kuwa kitamaduni, majukumu ya jinsia mbili katika familia ni changamoto kubwa kwa wanawake wakati wanapopigania usawa. Alisema kuwa mtoto msichana anapozaliwa anakuwa sikitiko kwa wazazi wengi.Mtoto msichana anathaminiwa kulingana na mahari itakayotolewa kwa wazazi wake. Kazi yake inatilia mkazo wazo la msichana kuthaminiwa kulingana na mahari aliyopewa mzazi.

Lugano (1989), anaonyesha juhudi za mhusika wa kike za kujikomboa zinavyokatizwa kutokana na maonevu ya kijamii yake. Wanadhulumiwa katika misingi ya nafasi wanazozichukua katika jamii na jinsi nafasi zao zinavyoweza kutumiwa kama misingi ya kufasiri maonevu. Anaeleza kuwa jukumu muhimu alilopewa mwanamke ni lile la uzazi. Kazi yake itatufaa katika utafiti huu kwani imeonyesha juhudi za mwanamke za kujikomboa zinavyokatizwa kutokana na maonevu ya mwanaume .

Tofauti na kazi hii, yeye anaonyesha juhudi za mhusika wa kike za kujikomboa zinavyokatizwa kutokana na maonevu ya jamii yake . Wanadhulumiwa katika misingi ya nafasi wanazozichukua katika jamii na jinsi nafasi zao zinavyoweza kutumiwa kama misingi ya kufasiri maonevu. Ameonyesha vile suala la udhalimu dhidi ya wanawake lilivyopewa kipaumbele na pumzi mpya za kuendeleza harakati zao. Kudhulumiwa kwa wanawake imepewa umuhimu mkubwa kiasi kwamba inamfanya mhusika wa kike kukubali kuwa hakuna jambo lolote linalomfaa isipokuwa kuolewa na kuzaa watoto. Lugano anasema kuwa asasi ya ndoa inaonekana kuwa mojawapo ya mbinu zinazotumiwa kumfanya mwanamke kuwa mtumwa wa mwanamume. Kazi hii ya Lugano inaonyesha mwanamke kutetea haki yake hasa pale mwanamke anapotambua kuwa anadhulumiwa.

Mule (1991) anaonyesha namna mwanamke alivyo mtegemezi wa mwanamume na jinsi ambavyo imemwia vigumu mwanamke kupata njia ambayo kwayo ataweza kujikomboa kutokana na baadhi ya mambo katika utamaduni wa Kiafrika . Jambo moja ambalo wahakiki hawa hawajalishughulikia kikamilivu ni matatizo

yanayowakabili wanawake na athari zinazotokanana matatizo hayo. Suala hili litashughulikiwa katika utafiti huu.

Swaleh (I992) alisema kuwa utamanduni ndio unaochangia kukandamizwa kwa mwanamke. Alishikilia kuwa dini ya Kiislamu inachangia katika nafasi anayowekwa katika jamii yake. Kazi yake inapinga dini ya Kiislamu kuchangia katika kumdhulumu mwanamke.Utafiti wetu unaunga mkono kazi ya Swaleh kwani udhalimu unatokanana mavazi wanayovaa wanawake.

Kurger (1998) Alilalamika kwamba ni vigumu kupata kazi za kifasihi ambapo wahusika wakuu ni wanawake. Mara nyingi huwa wahusika wajenzi. Hata hivyo mabadiliko yametokea na baadhi ya waandishi wamepatia wahusika wa kike nyadhifa muhimu katika kazi zao, kama; *Utengano (1980)*, *Tumaini* ( 2006), *Rosa Mistika* (1971), *Nguvu ya Sala* (1999), *Mwisho wa Kosa (*1987) n.k.

Momanyi, C (2001) alijikita katika suala la matumizi ya lugha. Alibainisha taswira ya mwanamke kama pambo, kifaa cha mwanaume asiyeaminika na anayenyenyekea katika matumizi ya lugha. Kazi hii ya Momanyi inatufaa kwa kuwa tunaangazia jinsi mwanamke anavyoweza kujinasua kutoka kwa dhuluma ya mwanaume kupitia usemi wake mwenyewe.

Katola, E (2006) aligusia masuala yanayomhusu mhusika wa kike kwamba mwanamke anadhulumiwa sana na anapewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Yeye anataja maonevu yote ya kimwili kama kuchapwa na kutawishwa yanayofanyiwa wanawake ambayo yamebainika katika utafitu wetu.

Traore , S (2008) alichunguza suala la familia na jamii katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kama, *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Asali Chungu* (1987) , *Tata za Asumini* (1990) na *Babu Alipofufuka* (2001). Katika uchunguzi wake alipata kuwa katika riwaya zote matatizo ya kifamilia na nafasi ya mwanamke ni masuala yanayosababisha matatizo makubwa kwa wahusika wa kike. Hii inadhihirika kupitia wahusika kama Maimuna katika *Utengano*, Semeni katika *Asali Chungu*, Asumini katika *Tata za Asumini* na Bi Kikuba katika *Babu alipofufuka* .Maudhui haya yamejitokeza katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na *Nyuso za Mwanamke* (2012). Maudhui haya yanamulika wanawake kama vile Dora, Zuhura, Lowela, Nana, Bi Mkubwa na wengineo.Sisi tumejikita katika uchunguzi wa wahusika wa kike na jinsi wanavyoathirika katika familia na jamii kwa jumla kutokana na uonevu wa wanaume na jamii.

Traore anachunguza wahusika katika muktadha wa kifamilia katika jamii. Ameonyesha namna ambavyo mifumo ya kifamilia na kijamii inavyowaathiri wahusika kimawazo.Uchunguzi huu unatusaidia kuchunguza wahusika wa kike na matukio yanayowapa hamasa kutenda wanavyotenda na athari ya vitendo vyao kwa wahusika wengine. Kwa mujibu wa mawazo haya, tumebaini kuwa wanawake wanapokabiliwa na matatizo wengi wao wanasumbuka kisaikolojia na hatimaye kuchukua hatua .

## 1.8 Njia za utafiti

Utafiti wetu kwa kiwango kikubwa ulikuwa ni wa maktabani.Tumetumia mbinu kadhaa kama vile kusoma riwaya teule kwa uzingatifu mkubwa ili tuweze kuzichanganua

vyema. Pili , tulidurusu vitabu, tasnifu na makala yanayohusiana na utafiti wetu. Tulifanya hivi ili kujiandaa kinadharia na vilevile kuyaelewa kwa undani masuala yanayohusiana na wanawake hususan matatizo anayokumbana nayo mhusika wa kike.

Pia tulijadiliana na wataalamu wa Nadharia ya Ufeministi tuliyoitumia ili kudhibiti ujuzi wetu. Juhudi hizi zilihakikisha kuwa utafiti wetu utategemezwa Nadharia tuliyoiteua.

## SURA YA PILI

## MATATIZO YA WANAWAKE KATIKA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA *NYUSO ZA MWANAMKE*.

### 2.0 Utangulizi

Mwanafasihi ni mwanajamii na ndiyo maana masuala yanayoendelezwa katika jamiihujitokeza katika fasihi. Fasihi kama kioo cha jamii haionyeshi sura ya jamii iliyotulia bali huonyesha sura ya jamii ya watu wanaoshughulika na kazi mbalimbali. Kile tunachokisoma katika fasihi huwa tunakifananisha na matukio ya kawaida katika jamii. Miongoni mwa yale yanayoshughulikiwa na taaluma ya fasihi ya Kiswahili ni udhalimu dhidi ya wahusika wa kike, tabia ambayo imedhihirika katika jamii.

Suala la haki na usawa kwa wahusika wa kike lina historia ndefu. Katika karne ya ishirini na moja ambapo suala la mwanamke katika jamii limepata umuhimu mkubwa.Baadhi ya wananadharia waliochangia katika nadharia za Ufeministi ni pamoja na De Beauvoir (1949), Millet (1977), na Eagleton (1986). Katika utafiti wao, wahakiki hawa walionyesha umuhimu wa ujenzi wa jamii mpya inayojali kuheshimu amali za kibinadamu kwa lengo la kuleta afueni kwa wanawake kama tabaka linalodhulumiwa katika jamii.

Walibora, K. (2012) na Mohammed, S.A (2010) wanatuonyesha mwanamke katika hali yake halisi ya kijamii na jinsi ambavyo utamaduni unavyomdhalilisha na kumweka katika nafasi ya pili baada ya mwanamume.Hata hivyo, mwanamke anayeangaziwa anatambua kuwa ananyanyaswa na hivyo anataka kujikomboa. Waandishi hawa

wanajitahidi kutuonyesha juhudi za wanawake kutaka kujiepusha na udhalimu dhidi yao. Jambo hili linaonyesha kwamba mwanamke wa Kiafrika ananyanyaswa na mwanamume na kwamba mwanamke huyu anaweza kujiepusha na udhalimu unaomkabili.Hii inabainika kupitia Nana katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*.
De Beauvoir (1949) alizishambulia taasisi za ndoa, dini na tamaduni ambazo zinachangia sana katika kudhulumiwa kwa mwanamke. Utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdhalilisha na kumfanya kuhusishwa na sifa hasi huku mwanamume akihusishwa na sifa chanya. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe wa mfumo wa jamii wa kuendeleza utamaduni huo hasi.

Katika sura hii matatizo ya aina mbalimbali yanayowakabili wanawake yamejadiliwa. Dhuluma hizo ni pamoja na kutusiwa ,ndoa ya lazima, dharau, kunyimwa haki za kuchuma mali na kuridhi, kutawishwa, dhuluma ya kimapenzi na kukengeushwa na jamii. Haya yote yamejadiliwa ili kubainisha kuwa hili ni suala linaloshughulikiwa katika riwaya zilizoteuliwa. Dhima kubwa ya fasihi ni ujenzi wa amali za jamii ambazo ni tamaduni, mila, desturi, dini, siasa na uchumi.

## 2.1 Ndoa ya lazima

Katika jamii nyingi za Kiafrika, hatima ya maisha ya mwanamke ni kuolewa. Jamii nyingi huchukulia mwanamke kama kiteka uchumi. Kabla ya kuolewa, ni lazima mali ilipwe kama dhamana.

Kulingana na Katola, E (2006) ndoa za kitamaduni katika Afrika zilipangwa na wazazi. Wazazi walikutana na kukubiliana kuwa watoto wao wafunge ndoa hata bila ya kuwauliza wala kuwafahamisha. Kaida za ndoa zilifuatwa kama vile kupeleka posa na baadaye kulipa mahari. Msichana hakuwa na hiari ya kukataa kwa hivyo aliishi na mtu ambaye hakuzijua tabia zake vizuri hali ambayo ilizipelekea ndoa hizi kukosa raha. Baadhi ya mambo yaliyotiliwa maanani katika uchaguzi huu ni pato la aliyeoa, jinsi familia hiyo ilivyohusiana na ile ya msichana, sura na tabia za msichana na hasa bidii yake.

Bi Mkubwa katika *Nyuso za Mwanamke* anamweleza bintiye Nana kwamba masomo yake yalikatishwa na kuingizwa katika Chuo kikuu cha ndoa ya lazima. Bi Mkubwa anasema hivi: "…*aliyenganganania babake apelekwe shule ambako alisoma mpaka darasa la kumi na mbili na baadaye kukatishwa masomo na kuingiza ndoa ya lazima". (uk290)*. Bi Mkubwa anaamua kujiepusha na ndoa iliyojaa dhuluma kwa kuondoka katika ndoa yao. Hata hivyo anapoolewa mara ya pili na ya tatu anazidi kudhulumiwa jambo ambalo hakulivumilia .Hii inadhihirisha kuwa wanawake wananyimwa haki ya kupata elimu.

Umebainika kuwa wanawake katika jamii ya riwaya tunazozishughulikia wanapinga wazo hili la dhuluma dhidi ya yao. Mfano wa hawa wanawake katika kazi tulizozishughulikia ni Nana, Bi Chuma, Bi Mau na Bi Mkubwa ambao wote wanaungana na kupinga vikali unyanyasaji kama huo.Mtunzi anawahimiza wanawake waungane na kuzipigania haki zao kwa kuzibadilisha sheria zinazosababisha kudhulumiwa kwao kama vile kuozwa kwa lazima . Umedhihirika kuwa suala la ndoa

na utajiri unachangia katika ukandamizwaji wa wanawake. Kwa hivyo wanawake wanahimizwa kulipuuza wazo la ndoa kuegemezwa kwenye mali na kumwunga mkono Steady (1981) ambaye yuko katika mstari wa mbele katika kutetea haki za wanawake. Mohammed,S. anawahimiza wanawake kubadilishwa kwa taasisi za kitamaduni zinazomkandamiza mwanamke na kumrejeshea utu na hisia zake za kibinadamu. Hii inabainika wakati Nana anapoamua kuondoka kwao na Bi Mkubwa naye kutengana na bwanake .Shemsa katika *Nyuso za Mwanamke* anaozwa kwa lazima. Yeye anaolewa na Sadiki ambaye hakumchagua mwenyewe. Shemsa anabaki kuwa mtumwa katika ndoa hiyo. Shemsa anaeleza hivi: "*...lakini matokeo ya ndoa yako ya kulazimishwa yamekuwa na matokeo gani kwako shemsa ...?"(uk* 211). Kwa kweli mwanamke kama huyu ataamua kuvunja pingu za ndoa yake na kumwacha mumewe.

Utafiti wetu umebaini kuwa katika baadhi ya jamii, mwanamke anaruhusiwa kujitafutia mchumba lakini katika jamii zingine anatafutiwa mchumba. Jamii nyingi pia huchukulia wanawake kama viteka uchumi. Kabla ya kuolewa ni lazima mahari itolewe kama dhamana.Hii inadhihirika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* .Bi Mkubwa anaeleza hivi: "*...alimwambia Nana kwamba licha ya kwamba yeye kaozwa Bwana Hila kwa nguvu za utajiri na mali (kwa sababu yeye hakutaka ) , bwana huyo ...". (*uk287 ). Hii inadhihirisha kwamba ndoa za lazima zilithibitiwa katika jamii za Kiafrika. Umebainika pia kuwa mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujitegemea na kukataa udhalimu dhidi yake. Bi Mkubwa anasema hivi: "*...haki yako ya uana jike itumie kwa busara, lakini dhuluma juu ya uke wako usiikubali..."(.uk 285).* Kauli hii inaonyesha kuwa kujiepusha na udhalimu si jambo linalowezekana kwa urahisi kwa

hivyo mwanamke anaweza kuishi vizuri bila ya kutegemea mwanamume.Ukweli huu unajitokeza pale ambapo Nana analazimika kumwacha babake na mamake wa kambo na kuishi peke yake.Anajiepusha na kunyimwa uhuru wake na pia kuozwa kwa mchumba anayechaguliwa na Bwana Hila.Mohammed, S.A (2010) anatuonyesha wahusika kama Bi Mkubwa,Nana na na Bi Mau wakijitahidi kupigania haki zao. Nana anaelezwa hivi: "...*Unataka kuolewa, hujui kwamba kuolewa ni kudhibitiwa na mwanamume*...?" (uk 286). Hii inaonyesha kuwa kuchaguliwa mume na wazazi na kuozwa bila hiari ya msichana ni njia ya kumdhulumu mwanamke. Hii ni kwa sababu kila mtu ana haki ya kujichagulia mwenziwe wa ndoa. Kigezo cha kutumiwa katika kufanya ule uchaguzi hakifai kuwa utajiri, hali ambayo inasababishwa na wanaume kuwa na haja ya mali bila kuzingatia maisha ya baadaye ya anayeolewa. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* mhusika mkuu ambaye ni Nana anaeleza hivi:

> *"... sitaki kuchaguliwa kama alivyochaguliwa mamangu… sita hofu kusema nampenda jini yule. Sita hofu kusema simtaki malaika yule . Ninapowaza hivi, huhisi moyo wangu umejaa hasira na kutaka kumkabili babangu kwa masuala magumu..." (uk 42) .*

Hii inaonyesha kuwa Bi Mkubwa alichaguliwa mume ambaye hakumchagua mwenyewe na Nana hangependa kufanyiwa vile mamake alivyofanyiwa.

Bw Hila, babake Nana anatumia kigezo hiki cha kumwoza bintiye kwa kuwa ana haja ya mali, yeye hajali maisha ya baadaye ya anayeolewa. Nana anaeleza kuwa

Dusa ni kijana mwenzake ndiyo, lakini hakumchagua. Amechaguliwa na babake awe mchumba wake na hatimaye awe mume wake. "... *Baba anayetaka kumwoza binti yake mume kwa zawadi ya Volvo..."(uk 44 - 45).*

Hii inaonyesha kuwa Nana anakerwa na wazo la kuchaguliwa mchumba.Kulingana na Katola, E(2006) anaeleza kuwa kuwaoza wasichana kwa watu matajiri ni aina ya udhalimu kwa sababu wao huishi maisha yaliyodhibitiwa na wanaume ambao kwao ni kama mabwana zao wanaostahili kuabudiwa.

Mwanamke kama huyu huishi maisha yasiyo na utulivu ambayo yanaongozwa na mtu mwingine na kukosa mamlaka juu ya maisha yake mwenyewe. Anakuwa mfungwa katika nyumba yake mwenyewe na anangojea tu kutolewa uamuzi kuhusu maisha yake.Hii inabainika wakati Shemsa katika *Nyuso za Mwanamke (2010)* anasema hivi*:*

> *"...hakunifanya bibi tokea mwanzo.Alinifanya mtumishi tu wa kuipikia familia nzima ambayo ina zaidi ya watu wanane watu wazima... Na si kupika tu..." . (uk 211).*

## 2.2 Kudharauliwa

Dharau ni tabia ya kupuuza na kutoheshimu watu. Dhana hii ya dharau imetumiwa ili kumtweza mwanamke. Kwa hivyo kudharauliwa kunajumlisha kutothaminiwa, kuvunjiwa heshima na kuaibishwa kupitia kwa vitendo vyakikatili dhidi ya wanawake. Mwanamke ana haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa kwani anachangia pakubwa katika maendeleo ya jamii kwa kutoa maoni na kuchuma mali katika jamii. Dharau inajitokeza pale ambapo mwanamke anakosa kudhaminiwa, kuvunjiwa heshima na

kuaibishwa kupitia kwa vitendo anayotendewa au lugha anayoelekezewa. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanawake* (2010) Fatuma alinajisiwa na mjomba wake akiwa mtoto mdogo na hata alipokuwa mkubwa. Hata hivyo mjomba mwenyewe alimtishia asiseme.Fatuma alipopata mimba, wazee wa ukoo huo walimsingizia kuwa aliipata mimba hiyo mahali pengine.Tunaelezwa kuwa yeye aliwatoa watu machozi pale alipohadithia jinsi alivyonajisiwa na mjomba wake na kuendelea. ‘‘... *Hakuna hata mmoja aliyethubutu kumkabili huyo mjomba*…” (uk 211) .Hii ina maana kwamba wanaume wanajiona bora zaidi kuliko wanawake .Hii ni kwa sababu ya mfumo wa ubabe dume.

Mtemi Nasaba Bora ambaye ni bwanake Bi Zuhura ni msaliti wa ndoa yake kwa kutembea na Lowela Binti Maozi huku akimwacha mke wake Bi Zuhura. Bw Mtemi Nasaba Bora anadhihirisha dharau kwa kutoheshimu ndoa yake. Zuhura anavunjiwa heshima na bwanake kwa kuwanyemelea mabinti za watu . Katika muda wa miaka mingi, Bi Dora na Mwalimu Majisifu wamekuwa wakiishi katika maisha ya ndoa yenye doa. Bi Dora anadharauliwa na mumewe kwa kuwazaa watoto walemavu. Bwana yake katika *Kidagaa Kimemwozea* anasema:

> *“...Lazima mwanamke huyu kafanya madhambi huko kwao alikotokea ndiyo maana ananizalia masharta haya ya binadamu. Mwanamke mjalaana asiyejua kuzaa wana ila hunikopolea tu ... ” ( uk 31*).

Hii inaonyesha kuwa mwalimu Majisifu anamdharau Bi Dora kwa sababu ni mwanamke.Huku kumlaumu Bi Dora kupata watoto walemavu inadhihirisha hali ya taasubi ya kiume. Wanaume ni nadra kutambua kuwa kuna uwezekano shida kama hii inatokana nao.

Mara nyingi mwanamke analaumiwa kwa kosa lisilo lake. Uduni wa wahusika wa kike unadhihirika na wanajikuta katika hali hiyo kwa sababu wanaume wanajiona bora na wasio na dosari yoyote.Bi Zuhura naye katika *Kidagaa Kimemwozea* (2010), anapewa talaka na mumewe Mtemi Nasaba Bora kwa kusingiziwa kuwa msaliti wa ndoa yao. Tunaelezwa kuwa Bi Zuhura alipata talaka asiyoiamkia wala kuilalia. Mtemi Nasaba Bora alifuka mno. *"...Nilidhani nimemwoa mke kumbe jamvi la wageni; Kila atakaye hulalia..." (uk 134).*Hii inadhihirisha kuwa mwanamke kwa sababu ya kudharauliwa anajikuta akirushiwa maneno machafu ya kumfedhehesha. Katika *Nyuso za Mwanawake (2012)* dharau linajidhihirisha wakati Bw Hila anamlaumu bintiye Nana kwa kusema hivi:

> *"...wewe u hali moja na mamako…Unatafuta unalotaka tu, lakini si lile analokuchukulia mtu anayekupenda maisha yako….Wewe unapita mguu uleule wa mamako..." (uk* 46- 47).

Kauli hii nayo inamtweza wanawake. Shemsa anapoelezea jinsi alivyohudumia Sadiki bwanake, hangeweza kuizuia michirizi ya machozi. Shemsa anasema kuwa

> alimfanya mtumishi tu wa kuipikia familia yake kubwa, familia nzima ambayo ina zaidi ya watu wanane wazima. Mamake, bibiake, babake, ndugu zake, marafiki zao--- na si kupika tu, bali kufua, kupiga pasi, kufagia, kutandika na kutandua. (Uk 211).

Hii inadhihirisha kuwa Shemsa ana uchungu mwingi kutokana na mateso na kunyanyaswa na bwana wake. Shemsa alitumikishwa kwa kila aina ya kazi na mumewe. Sadiki hapa, anamdharau bibiye na kuona kama hana thamana yoyote. Dharau hii inazorotesha uhusiano kati yake Shemsa na Sadiki. Hali hii inamfanya Shemsa kuitisha talaka.Shemsa anasema hivi: "*... Shemsa alishindwa kuyataja maneno ya mwisho, lakini yale aliyoyasema yalikuwa wazi kwa kila mtu kufikiri lolote baya sadiki alilotaka* kwa *Shemsa*. *Ilinibidi nidai talaka* ..." (uk 211). Hii inadhihirisha kuwa Mwanamke anakuwa kama mtumwa huku akitekeleza kazi zote kwa mujibu wa mgao wa majukumu katika jamii . Wanawake hawa wamejitahidi kupigania haki zao. Fatuma anajaribu kutafuta haki yake katika Korti wakati alinajisiwa na mjomba wake lakini anapuuzwa na wazee wa ukoo wanaomtetea mjomba wake. Shemsa, Fatuma na Nana wanapoamua kujadili mambo haya katika runinga wanahimiza wanawake wengine waungane pamoja ili kuukomesha udhalimu dhidi yao na wanadhihirisha ushujaa walio nao.Ushujaa wao unadhihirika wanapojinasua kutoka minyororo ya udhalimu na kuwahamasisha wanawake kupitia runinga. Bi Zuhura na wanawake wengine wanatuonyesha jinsi ambavyo taasisi ya utamaduni mkongwe unavyomdhalilisha mwanamke na kumweka katika nafasi ya pili baada ya mwanamume.

### 2.3 Dhuluma za kimapenzi

Kubakwa ni njia moja ya kumdhulumu mwanamke. Bi Mkubwa katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) ni mhusika aliyebakwa na mhindi.Tunaelezwa kuwa mhindi alimkamata kwa nguvu na kumbaka Bi Mkubwa. Bi Mkubwa alikwenda kushitaki polisi lakini alitiliwa huku na kutolewa kule, baada ya mkuu wa kituo cha polisi kula pesa za

mhindi. (uk 289). Hii inaonyesha kuwa utamaduni unampendelea wanaume kuliko wanawake.

Bi Mkubwa anapojaribu kutafuta haki yake katika korti baada ya kubakwa na mhindi, yeye anapata mdhulumu wake akiwa ametoa hongo. Hii inadhihirisha kuwa mwanamke anatazamwa kama kiumbe asiye na uwezo wowote . Bi Mkubwa anafahamu udhalimu anaotendewa wanawake. Anapomwandikia barua bintiye Nana anaonyesha kuelewa matatizo wanawake wanayoyapitia kutoka kwa wanaume.Anasema:

> " ... *Nimehakikisha kwamba nikutengenezee msingi wa kujitegemea kwa maisha yako ya baadaye, kwani mwanamke hawezi kuwa huru kama hana msingi wa kujitegemea kiuchumi. Utakuja wakati wa kujitetea na kuwakabili wanaume ana kwa ana . Sisi, mama zenu, tumekuwa tukipigana na dunia tofauti na yenu. Dunia ya kiume. Tumekuwa tukipigana na umwamba wa wanaume katika kila nukta ya maisha yetu mafupi..." (Uk 172-173).*

Hii inadhihirisha kuwa Bi Mkubwa anaelewa utamaduni unaomnyanyasa mwanamke.

Kauli hii inadhihirisha kuwa maoni na hisia za mwanamke hazitiliwi maanani.Uamuzi kama huu unamdhalilisha mwanamke . Naye mhusika Seleiman Kijogoo katika *Nyuso za Mwanamke* anamdhulumu Bi Mkubwa kwa kumfanya mtumwa wake.Tunalezwa hivi: "…*aliridhia utumwa wa kitandani na mwingine wa nje na ndani bila kulalamika*…"(uk 290) Seleiman Kijogoo alifanya hisia za Bi

Mkubwa kufifia katika mishipa yake . Seleiman alisababisha Bi Mkumbwa kuwa mgonjwa kiakili kwa sababu ya hamaki nyingi. Hali kama hii inamdhalilisha na kumfedhehesha mwanamke .

Bi Zuhura pia anadhulumiwa kimapenzi na bwanake Nasaba Bora kwa kumyima mapenzi ambayo anastahili kupewa. Ndoa baina ya Bi Zuhura na Mtemi Nasaba Bora imejaa mateso, unyanyasaji na kutoaminiana .Bi Zuhura ni mpweke na haja zake kutoka kwa mume wake hazikutimizwa. Mara kwa mara Mtemi Nasaba Bora anadanganya kuwa anakwenda kusuluhisha migogoro ya mashamba kumbe alikuwa anatembea na wanawake wengine kama Lowela binti Maozi . Bi Zuhura amekuwa katika hali ya kuvumilia kwa maovu ya bwanake. Anapopewa talaka na mumewe, mwandishi anatuonyesha mwisho wa shida kumwondokea mhusika huyu. Anapomtumia Bi Dora, anaonyesha pia vile alivumilia kwa muda mrefu katika ndoa yake . Yeye alivumilia ulevi, lugha ya karaha, ugomvi na uvivu wa mumewe. Hata hivyo wote wanatuonyesha kuwa mwanamume ndiye mkosaji.

Utafiti wetu umebaini kuwa hafai mwanamke kuendelea kuishi na mwanamume ambaye ni katili. Zaidi ya hayo, mwanamke anapojitenga na mumewe hafai kumrudia tena kwa sababu mwanamume huyo hataacha udhalimu wake.

Kulingana na utafiti wetu mwanamke atapata furaha na amani akiishi peke yake kama alivyofanya Nana.Wanawake wa Kiafrika wanaongezewa mzigo zaidi wa udhalimu na wanaume wa Kiafrika wanaowanyanyasa katika misingi ya kiutamaduni. Nasaba Bora ni mfano wa wanaume katika jamii nyingi za Kiafrika ambao hawachukulii mwanamke kama kiumbe sawa na mwanamume . Nasaba Bora

anamweka Bi Zuhura katika nafasi ya pili .Dhuluma za kimapenzi zinasababishwa na mfumo wa kuumeni, unaomtwaza mwanamume na kumtweza mwanamke.

Mtemi Nasaba Bora anamdhulumu Lowela Binti Maozi . Nasaba Bora anapokimbizana na msichana Lowela,ni njia moja ya kumharibu na hivyo kumdhulumu kwa kumtia mimba isiyo halali.Nasaba Bora anasema: "…*kama huyu ni mwanangu basi nilizaa na nani?... hilo halinihusu ndewe wala sikio. Ni haramu. Ndivyo alivyoitikia Mtemi Nasaba Bora ...*" (uk 41.)

Utafiti wetu unabaini kuwa ni vigumu kwa mtu yeyote kufahamu hali kama hii ya mtu anayewania kuwaharibu mabinti za watu. Haya yote yanaonyesha jinsi mwanamume anaepuka kuaibika hadharani kisha anamwacha mwanamke kubebeshwa aibu yote, huku mwenye kosa akiwa ametoweka kutoka katika uso wa jamii na kumwacha mwanamke akiandamwa na aibu.Inadhihirika kuwa wahusika wa kike wamo katika hali ya uchungu mwingi kutokana na udhalimu dhidi yao, na wasio tayari kuchukua hatua ya mara moja.

### 2.4 Lugha kama chombo cha kudhulumu

Lugha ya matusi inatumika kama njia moja ya kumdhulumu mwanamke na kumnyamazisha. Lugha ya matusi inamfanya mwanamke ajihisi duni kwani yanapotolewa na wanaume, hasa nia huwa ni kumdhalilisha na kumwonyesha jinsi ambavyo hana thamani yoyote.

Mwalimu Majisifu katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012:44-45), anapofika nyumbani usiku na kuanza kugombana na mkewe Dora, anamtusi huku akimwambia:

> *“...wataka mimi nipike? Ehee!...“ Bloody bastard! Shut up!...”wanawake wa siku hizi mmemea pembe. Unanijibu mimi kaa ...ma kama mwanamume? Basi nipe rinda nivae..e. Nipe rinda upuuzi kama huu kazungumze na wanawake wenzako… nikome kama ulivyokoma titi la mamako...”( uk 44_45).*

Kauli hii inaonyesha mwanamke kudunishwa kupitia lugha inayotumiwa na wanaume. Matusi kama hayo pia yanaelekezwa kwa Bi Zuhura bibiye Bwana Mtemi Nasaba Bora. Haya ni maneno yanayoelekezwa kwa mwanamke na mwanaume.Hapa mwanaume anamdhulumu mwanamke kwa kumzuia mambo yanayoweza kumvunja mwanamke , kumwaibisha na kumdhalilisha. Hali hii inatokana na ule ukandamizaji wa mfumo wa kuumeni uliopata mizizi katika jamii nyingi za Kiafrika kiasi cha kuudumisha utu wa mwanamke.

Naye Lowela binti Maozi anamtukana Bi Zuhura .Matusi haya yanatolewa na msichana ambaye wanasema kuwa ameharibika.Haya ni maneno yanayoelekezwa kwa mwanamke na mwanamke mwenzake . Hapa mwanamke anadhulumiwa na mwanamke mwenzake. Lowela Binti Maozi anasema kuhusu Bi Zuhura katika barua aliyomwandikia Mtemi Nasaba Bora “*...je, kweli nalinganishwa na yule ajuza wako mwenye manyama tembweretebwere kama ya nguruwe?” (uk 105-106).* Lowela anapotamka hayo anaonyesha kwamba ni mpotovu kinidhamu kwani anamkashifu Bi Zuhura katika barua yake kwa Mtemi Nasaba ingawa yeye ndiye aliyeingilia ndoa ya wenyewe . Udhalimu unaofanyiwa wanawake na wanawake wengine unasababishwa na

ukosefu wa uhuru wa kibinafsi unaowafanya baadhi ya wanawake kuwa na mielekezo hasi kuhusu maisha yao. Hapa mwanamke mwenyewe ni tatizo kubwa kwa mwanamke mwenzake. Steady (1981) anashikilia kuwa wanawake wa Kiafrika pamoja na matatizo mengi yanayowakabili yalitokana zaidi na utamaduni na wao wenyewe walichangia pakubwa katika ule unyanyasaji unaowakabili.

Katika *Kidagaa Kimemwozea (2012)* Nasaba Bora anadhalilisha Bi Zuhura kwa kumkaripia kwa maneno yake makali.Kutoka na lugha ya kudhalilisha, ilibidi Zuhura mkewe afuate masharti yake bila pingamizi. Imani katika *Kidagaa Kimemwozea (2012* ) anatusiwa na askari wa Mtemi Nasaba Bora.Askari anasema hivi: "*Nyamaza boza wewe . Wadhani sisi kazi tunaanza leo? "Tumekutana na wauaji wangapi? Yatazame macho yao yanavyopepea kama wauaji sugu kabisa"(uk 84*) Wanawake hawa wote wanaotusiwa ni mfano wa wanawake wa Kiafrika wanaochukua hatua ya kufuata njia pekee ambayo itawaondolea udhalimu unaowakabili kama vile Nana anapochukua hatua ya kuondoka. Hata hivyo, kunga'nga'nia ukombozi sio jambo rahisi kwani wanawake wanakabiliwa na vitisho na kunyamazishwa kwingi ambako kunawakatiza tamaa.

### 2.5 Kutawishwa

Kutawishwa ni hali ya kuwafungia wanawake ndani ya nyumba kwa nia ya kutotakiwa watoke nje ili washirikiane na wanaume wasio wanaume zao na kuhakikisha kwamba wanawake wamewekewa mipaka. Utawa una asili yake katika dini ya Kiislamu na kama Momanyi (1998) anavyosema, huhusishwa na maandiko kutoka Kurani Takatifu. Nia ya kutawisha wanawake ni kule kuwafungia kwa kuhofia kwamba wakiachwa huru

watatembea na kufanya mapenzi na wanaume wasio mabwana zao. Hii ni kwa sababu mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu. Katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) Nana anatawishwa ili asitoke nje na kukutana na wanaume. Bwana Hila, ambaye ni babake Nana anaeleza kwamba Nana bado ni mwanagenzi wa dunia.

Bwana Hila anashikilia kwamba lazima amhifadhi Nana hasa kwa vile bado ni msichana ambaye hajapata mume bado mdogo tu. Asingekubali kumwacha kuzurura ovyo na kuwa windo rahisi la masimba na mafisi yanayozurura jijini na mitaani.(uk 38).

Miaka ya mwanzo, Nana alipelekwa na kurudishwa nyumbani kutoka shule kwa gari. Hii inaonyesha kuwa Bw Hila alitaka Nana asije akaharibiwa na wanaume. Hata hivyo Nana anaenda kinyume na matakwa ya babake. Nana anataka haki yake ya kuwa huru. Nana anasema kuwa si mtoto mchanga tena. Anataka kujifunza kuwa peke yake na dunia yake.Kulingana na Mohamed,S (2010) inadhihirika kuwa jamii za Afrika ina matarijio fulani kwa mtoto wa kike hasa kabla ya kuolewa. Wazazi wake wanavutika kuchukua hatua fulani kuhakikisha kwamba wamemlinda binti yao. Naye Bi Mkubwa anatawishwa na Bw Hila.Nana anaelezwa kuwa:

> “ … *Sitaki kuwa kamwe mwanamke kama mamangu wa kambo, au mwanamke anayefyozwa damu taratibu huku akimalizika kama mamangu mzazi” (uk 108).*

Kauli hii inadhihirisha kwamba bwana Hila alidhani maisha ya mwanamke ni kustarehesha mwanamume tu. Desturi ya ndoa katika jamii nyingi za Kiafrika ina matarajio fulani kwa wahusika wote wa kike .Kutokana na kutawishwa kwa

mwanamke¸ familia inakuwa ni asasi ambayo imetumiwa kuhalalisha udhalimu. Imebainika wazi kwamba asasi ya ndoa inachangia pakubwa katika kueneza dhuluma dhidi ya mwanamke. Katika muktadha huo sio wanawake wengi waliopewa fursa ya kujiamulia wachumba waliowataka bali uamuzi ulifanywa na wazazi. Moja kati ya mambo ambayo mwanamke hatarajiwi kujiamulia ni uchaguzi wa mchumba amtakaye.

Katika *Kidagaa Kimemwozea* (2010) Dora, ambaye ni bibiye Mwalimu Majisifu anatawishwa kwa mujibu wa kutunza watoto wake walemavu ilhali bwanake analewa kila siku.Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mwenye majukumu yanayomfunga nyumbani na hivyo hana sababu yoyote ya kumfanya atoke nje kama mwanaume.Haya yanajidhihirisha katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* wakati Bi Dora anasema hivi; "…*kazi zimenilemea na kunisonga*. *Mwenyewe unalaza hupiki hupakui*.*Unachojua ni kulewa tu...*" (uk 44).

Naye Bi Zuhura bibiye Mtemi Nasaba Bora anajipata katika hali hiyo ya kustawishwa kwa wanawake.Ndoa inakuwa ni taasisi ambayo imetumiwa kuhalalisha udhalimu hasa kwa wahusika wake. Bi Zuhura anasema:

> "…*Mume ajaye usiku wa manane au jogoo la kwanza na kujibwaga kitandani kama gogo la mti ni mume gani?... alijiona maskini katikati ya mali isiyodirika. Alikuwa na kiu, lakini si ya maji. Alikuwa na njaa lakini si ya chakula" (uk 90-91*).

Hii inaonyesha kuwa Bi Dora anauchungu mwingi na hivyo kusumbuka moyoni. Kauli hii inadhihirisha kuwa wanawake wanajipata katika hali ya ukiwa kutokana na udhalimu huo.

## 2.6 Kunyimwa haki za kuchuma mali na kurithi

Udhalimu mwingine unaofanyiwa wahusika wa kike ni ule wa kuwanyima haki za kuchuma na kurithi mali.. Katika baadhi ya jamii za Kiafrika, hasa katika riwaya tuliyoshughulikia wanawake wananyimwa haki za kumiliki mali au kujieleza kwa vyovyote. Wanawake katika jamii za jadi hawakushirikishwa katika kufanya kazi za uzalishaji mali. Kazi zao ni za kinyumbani na haziwasaidii kupata pato lolote. Wanawake katika riwaya tulizoshughulikiwa katika tasnifu hii ndio wanafanyishwa kazi zote za nyumbani kuzitekeleza huku waume wakistarehe.Tunaelezwa hivi:

> *"…Maisha yetu wanawake hapa petu yamefinyangwa ndani ya tamanduni zilizoasisiwa na mwanamme ambazo bado zina nguvu kupita kiasi … Mimi licha ya kutotaka kubaki jikoni na kupakua, kuosha vyombo na kufagia na kutunza watoto, sitaki kamwe hata kuwa mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamume"(uk 107).*

Kauli hii inadhihirisha kuwa ni lazima wanawake wajitahidi kufanya kazi zinazofaa kuitwa zao huku wakipana moyo katika maisha yao yenye kuchosha sana.

Kulingana na Ogundipe-Leslie (1984), anasema ni mwanamke mwenyewe anafaa atambue kuwa yeye tu ndiye anayeweza kupata uhuru wake na kujua kile hasa anachohitaji.Hii inadhihirika katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) ambapo wanawake wanadhihirisha ushujaa . Ukweli huu unadhihirika pale ambapo Nana anaamua kujiunga na Bi Mau na Bi Chuma ili kuanza maisha mapya ya kjitegemea. Jamii inahitaji kumpa mwanamke nafasi kujiamulia maisha yanayomhusu.

Kati ya mambo yanayochangia udhalimu dhidi ya wahusika wa kike wa Kiafrika ni tamanduni. Tamaduni nyingi za Kiafrika zinamdunisha mwanamke na kumfanya kama kiumbe cha kutoa huduma kwa wengine hasa mumewe na watoto. Hakuna wa kumshukuru au kumpongeza bali anatusiwa na kukanwa kama Bi Dora na Bi Zuhura katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012).

Bi Mkubwa, mamake Nana kwa sababu ya kukosa uwelewano ndani ya nyumba na bwanake, anaamua kutengana na bwana Hila ili aweze kutafuta uhuru. Yote yanayomfikia mwanamke yanatokana na nafasi aliyopewa katika jamii za Kiafrika.Katika jamii hizi, mwanamume ndiye anategemewa na mkewe hana budi kuyafuata maagizo yake. Wengine wanaojipata katika dau kama hilo la Bi Mau na Bi Mkubwa ni pamoja na Bi Chuma.

Mamake Imani ananyimwa haki yake ya kumiliki shamba la hayati mumewe. Anadhulumiwa kwa kunyanganywa shamba la mumewe. Hata hivyo Mamake Imani anapata upinzani mkali kutoka kwa askari wa Mtemi Nasaba Bora kwa kuleta hatimiliki ya shamba isiyo halali. Mamake Imani anakata roho kutokana na kipigo alichopigwa na askari.Tunaelezwa hivi:

> "*Wametumwa kumwondoa mama na aila yake katika shamba la mwenyewe . Mama akawauliza tena mwenyewe ni nani hawakumjibu wakacheka ...wakatoa hati nyingine ya shamba hilo ...walimpiga kitutu kama nyoka". (uk 58)*

Hii inatuonyesha juhudi zinazochukuliwa na wanawake kijikomboa na labda kuisahihisha jamii.Utafiti wetu umebaini kuwa wanawake wanaonekana kulalama na kujinasua kutoka minyororo ya udhalimu kwa haraka. Tunaonyeshwa mamake Imani akiwa anapigania haki ya kumiliki mali ya mumewe ambaye alikuwa hayati.Yeye anakataa katakata kuachilia shamba lake la Baraka.

Bi Dora mkewe Mwalimu Majisifu Majirefu anadhulumiwa na mumewe kwa ulezi mzito wa watoto wao punguani na walemavu. Bi Dora anakaripiwa kwa lugha isiyofaa na mumewe anapojaribu kumkumbusha kuhusu jukumu lake la ulezi .( uk 60) . Umebainika kuwa wanawake kama Nana, Bi Mkubwa, Bi Dora, Bi Zuhura na wengine katika kazi hii wanadhulumiwa.

## 2.7 Kukanwa na jamii

Wanawake wanapoteleza tu, jamii inakataa kuwakubali tena na kuwaona kwamba ni watu wanaofaa kutengwa kutokana na imani kwamba eti wanaiaibisha jamii. Nana katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) anaamua kujitafutia uhuru wake, harudi kwao, mpaka wakati babake anakuwa mgonjwa mahututi. Nana anajawa na woga asijue la kufanya anapogundua kwamba babake ndiye alimfanyia njama ya kuteketeza nyumba yake.

Nana anakanwa na babake kwa kukataa uamuzi wake wa kumchagulia mchumba. Bwana Hila anamweleza Nana kuwa yeye ni kama mamake. Tunaelezwa hivi: "...*Wewe sawasawa na mama yako, aliniambia...Sijui kwa nini zimenijia chuki juu yao kiasi hicho...*" *(uk 49)*

.Nana anaonekana kuwaacha watu wa familia yake ili aweze kuishi maisha ya uhuru. Bila shaka msichana asiye na hatia amekanwa na babake mzazi. Bwana Hila katika *Nyuso za Mwanamke* anamkana Bi Mkubwa kwa sababu ya kutoelewana katika ndoa na wanatengana. Bw Hila anamkana Bi Mkubwa kwani Bwana Hila alidhani maisha ya mwanamke ni kustarehesha . Anachostahili ni kupewa kila kitu anachokitaka, lakini Bi Mkubwa anahitaji uhuru wake. Hali kama hii inasababisha utata katika ndoa.

Utafiti wetu umedhihirisha jinsi wanawake wengi wanavyojaribu kujiepusha na udhalimu dhidi yao na kuwashawishi wanawake wengine kujitokeza na kupigana na hali inayowakabili. Kulingana na riwaya tulizozishughulikia tunaonyeshwa Nana akiamua kuanza safari mpya ya maisha yake , ilikujiimarisha kiuchumi.( uk 57). Bi Mkubwa, naye anaamua kuishi nyumba ya kupanga baada ya kutengana na bwana

Hila. Hata hivyo hajaridhika ndiposa anamwandikia barua bintiye ya kumwonya kuwa angetaka bintiye ajitegemee kiuchumi siku zake za baadaye. (Uk 172)

Katika jamii yenye mfumo wa kuumeni, mwanamke hukengeushwa na hali halisi inayomzunguka kiasi cha kutouona uhasi wa jamii yake kumhusu. Jamii humtumia mwanamke kama nyenzo kuu ya kuiendeleza ile itikadi au imani ya nafasi yake duni kama kiumbe. Si ajabu Bi Mkubwa anamwandikia bintiye barua kuhusu maisha yake ya baadaye kama mwanamke. Pengine huu ndio msimamo wa Mohammed, S.A (2010) kama mwandishi. Utafiti umebaini kuwa wanawake wajikomboe kutokana na utamaduni wa jamii yake. Pia wanamke wanahimizwa kuchukua hatua ya kundoka katika jamii inayodhulumu na kwenda kushirikiana na walio tayari kujiendeleza kwa madhumuni ya kujenga kizazi kipya.

Katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012) Bi Zuhura anakanwa na mumewe Bw Mtemi Nasaba Bora anapomshuku Bi Zuhura kuwa si mwaminifu, anampa talaka mara moja. Kitendo hiki cha kumpa talaka Bi Zuhura kinawafanya watu wa Sokomoko kushangaa kwa nini anamtaliki mkewe mwaminifu aliyeishi naye kwa stahamala miaka nenda mia rudi. Talaka yenyewe haina msingi thabiti kwani Bi Zuhura hakulitenda tendo la kimapenzi na Amani .Tunaelezwa hivi:

> “ *...Nyumbani kwa Mtemi Nasaba Bora, Bi Zuhura*
> *alipata talaka... Naye Bi Zuhura akajisemea*
> *kimoyomoyo, “ Kwa miaka nenda*
> *miaka rudi mwanamume mwenyewe*
> *kanitumia kama kopo la msalani...*”(uk 134) .

Mwanamke ambaye anaonekana kuwa mfungwa katika nyumba yake ndiye anayekanwa na yule anayefaa kumjali na kuwa naye karibu. Mwanamke anapata fedheha baada ya kukanwa, anaona jambo la kufanya ni kujitenga na anayemfedhehesha na kumdhalilisha. Mfano wa wanawake kama hao ni pamoja na Nana, Bi Mkubwa na Bi Zuhura.Kutokana na haya unabainika kuwa wahusika wa kike wanakanwa na jamii kwa kuchukuliwa kuwa wanaiaibisha kwa vitendo vyao.

### 2.8 Hitimisho

Sura hii imejadili aina mbalimbali za udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kama zinavyojitokeza katika riwaya zilizoteuliwa na mtafiti. Wazazi wa kiume hupenda kuhusishwa na watoto wenye tabia njema wala sio wenye tabia mbaya. Wanaokanwa wanakabiliwa na shida ya kujitambulisha wasijue wajihusishe na nani. Wanawake wanaotengwa na wanaume zao wanaamua kujitenga pia kwa kujitafutia makao au kurudi kwa wazazi wao. Wanawake wanafanywa waishi katika hali ya woga na hofu kwa kutojua kitakachotokea baadaye. Udhalimu huu unaosababishwa na kule kutaka kuhusika na wanaume na kujulikana kuwa wao ndio wenye mamlaka juu ya maisha ya wanawake na wanaweza kufanya lolote

Wasichana wanaozwa bila wao kutaka au kabla ya kuulizwa na wazazi hasa wanatarajiwa wawakubali kama waume zao. Mfumo wa kuumeni ndio unaosababisha hali hii kwani mwanamke haangaliwi kama binadamu aliye na hisia na anayeweza kujiamulia mwenyewe utaratibu wa maisha yake.

Kudharauliwa ni aina moja ya udhalimu wanaotendewa na wanaume. Katika jamii nyingi, mwanamke anasemekana kuwa ana akili dhaifu na hawezi kutoa uamuzi wowote wa maana, huchukulia kuwa hana nguvu za kimwili, ni mnyonge kwa kila njia.

Udhalimu mwingine unaokabili mwanamke ni kutukanwa. Matusi humshushia heshima mwanamke. Endapo mwanamke ataenda kando ya matarajio ya mwanamume anatukanwa na hivyo kuaibishwa.

Udhalimu mwingine unaofanyiwa wanawake ni kutawishwa , kufungiwa ndani ya nyumba na kutotakiwa kuonana na yeyote isipokuwa watu wa familia yao. Hivyo ni kumdhulumu mwanamke. Wanawake wamenyimwa haki ya kumiliki mali na pia uhuru wa kutoa maoni kwa sababu ya imani na mila za kitamaduni. Mfumo wa kuumeni umesababisha kuendelezwa kwa dhuluma hii kwani unapoendelea wanaume wanawapa wanawake nafasi ya pili bila ya msingi yoyote dhabiti.

Ilidhihirika wazi kuwa baadhi ya wanawake wa Afrika wamejitahidi na kuwa na hekima ya kujiondoa katika udhalimu huo na kuthibitisha kuwa na uwezo wa kujitegemea na kutoa uamuzi ufaao. Hivyo basi, wanawake si viumbe duni wenye udhaifu wa kiakili. Imebainika pia kwamba waandishi wamethibisha utambuzi wa nadharia ilioongoza utafiti huu kwamba mwanamke wa Kiafrika anakabiliwa na udhalimu,kutoka kwa mwanamume na kwamba utamaduni wa Kiafrika unachangia pakubwa kuweko kwa udhalimu huu . Aidha mwanamke wa Kiafrika atahitaji kujielewa kwanza ili ajiondoe katika nafasi duni . Nadharia hii ya Ufeministi inawahimiza wanawake waungane na kushirikiana katika kupambana na udhalimu dhidi

yao wanaofanyiwa na wanaume.Wakifanya hivi wanaweza kujikuza na kujiendeleza kama wenzao wa jinsia ya kiume.

## SURA YA TATU

## ATHARI MBALIMBALI ZINAZOTOKANA NA MATATIZO YANAYOWAKABILI WANAWAKE.

### 3.0 Utangulizi

Sura hii imejikita katika kuchunguza na kueleza athari za udhalimu dhidi ya wahusika wa kike . Kulingana na Wamitila,K W (2003) Kazi ya fasihi si ya kuyaeleza yaliyo mema na yapendwao kusikiwa,bali ina jukumu la kuyaeleza hadharani hata matendo yale maovu yajulikane ili kutafutiwa suluhisho.Mwandishi haishi kwa kuyaeleza yale yalioyo wazi tu, bali kuyaonyesha jamii hata yale yasiyo wazi ili kuwazindua wanaopitia katika matatizo mbalimbali ili waweze kujikomboa . Ni muhimu basi kuchunguza athari za udhalimu dhidi ya wahusika wa kike ambamo mwanamke anajikuta na namna anavyojitahidi kujiepusha na maisha haya ya unyanyasaji . Wahusika wengi wa kike katika fasihi ya Kiswahili wanakabiliwa na udhalimu unaotokana na vitendo vya wanaume. Kwa mujibu wa wahakiki Birke (1986) , Lovenduski na Randall (1993) wanaeleza kwamba, mwanamke wa Kiafrika anaweza kujitegemea na kuishi bila ya kunyanyaswa.Pia anaweza kuwa shujaa na ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii ambayo yeye ni mshiriki.

Athari zitakazochanganuliwa ni zile ambazo zimejitokeza katika riwaya mbili zinazoshughulikiwa, *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Athari hizo ni pamoja na kusambaratika kwa ndoa, kukata tamaa, woga, mauti, upweke

na uhusiano wa kinyumba.Athari hizi zitaelezwa kama zinavyojitokeza katika riwaya moja baada ya nyingine.

Utafiti umeonyesha wahusika ambao wameishi katika dhiki kwa miaka mingi. Bi Zuhura na Bi Dora wamekuwa wakivumilia kwa yote yaliyowapata.Wanavumilia kwa yote yaliyowapata kutokana na vitendo viovu vya waume zao. Bi Zuhura na Bi Dora hawatoroki na kuwaacha wanaume hawa, kama walivyofanya Nana na Bi Mkubwa. Bi Zuhura anavumilia maovu ya Nasaba Bora lakini mwishowe anapewa talaka.Umebainika kuwa wanaume wanasawiriwa kama watu ambao hawako tayari kusikiliza mawaidha yoyote kutoka kwa wanawake. Hata hivyo imebainika kuwa iwapo ndoa haiwezi kumletea mtu furaha maishani,hana budi kuivunja.

**3.1 Kusambaratika kwa ndoa**

Udhalimu unaotendewa mwanamke unasababisha ndoa kukosa lengo lake kwa wawili walioona ili waishi kwa umoja. Ndoa yao inakosa ladha na kutawanyika wasiwe na mshikamano. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) Bi Mkubwa anaishi maisha magumu na yaliyojaa mateso kutoka kwa mumewe Bw. Hila. Bi Mkubwa anapoona hapati raha katika ndoa yake analazimika kuondoka kwake na kwenda kuishi katika nyumba ya kupanga. Ndoa ya aina hii huwa imepoteza ladha yake na huwa haiwafaidi wahusika. Bw Hila anaamini kuwa maisha ya mwanamke ni kustareheshwa, kupewa kila kitu anachokitaka apewe mawazo ya kifahari na yeye kama mwanamke abaki kungoja kumstarehesha Bwana na kubaki ndani ya nyumba. (uk 287). Kitendo hiki cha kumwacha mwanamume huwa mara nyingi ndicho kinachowaokoa wanawake kutokana na lindi la udhalimu wa bwana zao.

Ni baada ya kuondoka kwa wanawakei ndipo wanaume wanafahamu umuhimu wa kuwepo kwa wake zao. Baada ya Bi Mkubwa kuondoka Bw Hila anaoa bibi mwingine.Ukweli ni kwamba, nyumba bila mke haiwezi kuwa na joto na bashasha.

Hali ya kutokuwa na masikilizano kati ya bwana na bibi imewafanya kuwa na mtoto moja ambaye ni Nana. Bi Mkubwa anapoamua kuondoka, anaamini kuwa Nana ambaye ni bintiye atakuja kupata wakati wake wa kujitetea, kisiasa na hata kujikimu kiuchumi. Anasema hivi: *"...Sisi, Mama zenu, tumekuwa tukipigana na dunia tofauti na yenu. Dunia ya kiume..." (uk*172).

Umebainika kuwa wanaume wengi wa Kiafrika wanaongozwa na imani kwamba mwanamke anapoolewa na kutoshelezewa mahitaji yake yote, anafaa kuridhika. Hili linadhihirishwa na Bw. Hila. (uk 287). Wanaume hawa wana mali, utajiri na wako katika harakati za kuchuma mali zaidi. Wanaume hawa wananyima wake zao mapenzi na hatimaye wake hawa wanachoshwa na maisha ya ukiwa na wanaamua kuondoka. Bi Mkubwa anapoolewa mara ya pili na Bw. Simai, mchezo wa udhalimu ni ule ule. Baada ya muda mfupi tu wa kuolewa na Simai, Bi Mkubwa alitambua kuwa amekutana mwanaume anayependa kupiga wanawake. Bi. Mkubwa alifahamu kuwa ile haikuwa ndoa, ila ni kadhia ya mwanamke kufunzwa na ulimwengu. Bi. Mkubwa alifunga virago vyake na kuelekea kwenye kitovu cha jiji hilo. Anapoajiriwa katika duka la mhindi, anabakwa na mhindi mwenyewe. Bi Mkubwa hangeweza kuvumilia katika ndoa zake zote. Kitendo cha kumwacha mwanamume huwa mara nyingi ndicho kinachowaokoa wanawake kutokana na udhalimu dhidi yao.

Naye Nana, mhusika mkuu katika riwaya hiyo anatoroka kwao ili ajipatie uhuru wake binafsi. Kitendo cha Nana kutoroka, kinafanya familia ya Bw Hila isambaratike.Nadharia ya Ufeministi unaoongoza utafiti huu unadhibitisha kwamba mwanamke wa Kiafrika anaweza kujitegemea maishani.

Hii inadhihirisha kuwa ndoa yenye doa inaleta athari hasi kwa wanaohusika na inakuwa ni vigumu kuishi kwayo.Nadharia inahimiza kubadilishwa au kuuondolewa kwa baadhi ya taasisi za kijamii zinazotumiwa kumdhulumu mwanamke kama vile mali katika asisi ya ndoa. Ingawa Bi Mkubwa aliondoka katika ndoa, hakuweza kufikiria kuhusu mtoto wake Nana ambaye alihitaji upendo wa mamake. Nana aliathirika kutokana na kusambaratika kwa ndoa kati ya mama yake na baba yake.

Utafiti umebaini kuwa kuna wanawake ambao ni mashujaa na jasiri. Wanawake hawa wanaamua kuchukua hatua ya kuondoka na kuwaacha jamaa zao. Hatimaye imedhihirika kuwa mwanamume ndiye mkosaji.Bi Mkubwa katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) anawaacha wanaume wote waliowahi kumwoa kila anapodhulumiwa. Mara ya kwanza Bi Mkubwa anatengana na mume wa kwanza ambaye ni bwana Hila. Bi Mkubwa anamwona kama anamdhulumu. Mara ya pili anaolewa na mume ambaye kiboko kilikuwa kiamsha kinywa chake.Tunaelezwa hivi: "...*Bi Mkubwa akaanza kuhadithia maisha yake na waume na maisha yake ya ndoa. Mwanamke ni pambo tu la nyumba kwa hivyo anachostahiki ni kupewa kila kitu alichokitaka isipokuwa kutoka nje ya nyumba.Apewe mavazi ya kifahari, manukato ghali, chakula cha rutuba, watumishi, gari la kusafiri na bwana*..."(287). Umebainika kuwa matatizo yanayoangaziwa katika utafiti huu ni kuwa matatizo katika ndoa yanaweza kuwa yanasababishwa na kiwango cha elimu kwa upande wa wahusika.

Utafiti umeonyesha kwamba mwanamke si lazima amtegemee mwanamume. Hii inadhihirika kupitia Nana na Bi Mkubwa wanawaacha jamii zao mara tu wanapogundua kwamba wanadhulumiwa. Katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012), Bi Zuhura ni mfano wa mwanamke aliyeolewa na mwanamume mtaka makuu. Mwanamume kama huyu huwa anamchukulia mke wake kama chombo cha kutumiwa tu. Tabia ya Mtemi Nasaba Bora kuwa na jicho la nje limezorotesha masikilizano kati ya mume na mkewe. Kinyume na Bi Mkubwa, Bi Zuhura anaamua kuvumilia katika ndoa isiyo na furaha. Bi Zuhura anamshuku bwana yake Nasaba Bora kuwa ni msaliti wa ndoa lakini afanyaje? Tunaelezwa hivi: "… *Bi Zuhura katika Kidagaa Kimemwozea* (2012) *hakudadisi zaidi udhuru wa mumewe wa cheleo la kila siku uliokuwa wimbo uliozoelewa*." (uk 55) Ndoa ya Bi Zuhura inasambaratika hata ingawa anajaribu awezavyo kuvumilia ili aidumishe. Ana uchungu mwingi, hasa anapokumbuka yale anayotendewa na bwana wake. Imani ya Bi Zuhura katika ndoa imepotea kabisa kwani kwake ni kama mtumwa wa kimwili. (uk 55).

Bi Zuhura aliolewa na mwanamume ambaye si mwaminifu katika ndoa. Mumewe bwana Nasaba Bora ana wanawake wengine na hata Lowela bintiye Maozi anamkashifu Bi Zuhura katika barua yake kwa Nasaba Bora. Lowela anasema:

> "*... Hebu litazame umbo langu na umri wangu na haibu yangu.*
> *Je, kweli nalinganishwa na yule ajuza wako mwenye*
> *Manyama tembweretembwere kama ya nguruwe?"*

Ni tabia ya Bw. Nasaba Bora ya kuwa na wanawake nje ya ndoa inayomfanya Bi. Zuhura kuwa na uchungu mwingi moyoni mwake. Hata hivyo anavumilia katika ndoa isiyo na furaha.

Anaelewa fika kuwa familia inamhitaji na yuko tayari kumkabili mumewe na kumweleza yote. Ingawa si rahisi Bw. Nasaba Bora kukubali makosa yake, BiZuhura anajikakamua kujitetea. Mtunzi anasema anasema:

> *"… Bi Zuhura alipolaza katika kitanda chao chenye matendegu ya msonabari na godoro lenye maki pana, alitafunwa na ukiwa na jaka moyo." (uk 90).*

Hali hii humwathiri mwanamke kisaikolojia na kihisia.Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) tuonyeshwa vile Bi Zuhura anavyojitoa kuvumilia katika ndoa. Anaoyesha uvumilivu wa hali ya juu ambapo anagundua kwamba mumewe hampendi kwa sababu alikuwa na wanawake wengine huko nje. Mwishowe Bi Zuhura anatalakiwa na mumewe bwana Mtemi Nasaba Bora.Mwanamke anasawiriwa kama mtu duni anayemtegemea mwanamume kulingana na utamaduni unavyowaongoza. Kwake mwanamke ataendelea kukaa na mwanamume hata kama uhusiano mwema haupo. Katika utafiti wetu inadhihirika kwamba wanaume katika jamii nyingi wana maoni tofauti kuhusu ndoa kama Bw. Nasaba Bora, wanachukuliwa kuwa mwanamke hana haki ya kudai chochote au hata kutoa maoni yoyote hasa ya kueleza kutoridhika kwake. Mume anajiona kama mwenye mamlaka kwa kila jambo. Bw. Nasaba Bora anafika nyumbani usiku wa manane au jogoo la kwanza. Maelezo ya Bi Zuhura kuhusu bwana yake, ni kwamba ni mume mkali ambaye asemezeki wala haambiliki hasa na mwanamke kama yeye.

Kutokana utafiti wetu inadhihirika kwamba jamii nyingi za Kiafrika zina falsafa tofauti kuhusu ndoa.Katika jamii za jadi kuna wale wanaochukulia kuwa mwanamke

anapoolewa na kutolewa mahari anakuwa mali ya mwanamume na hana haki ya kudai umiliki wa kitu chochote au hata kuruhusiwa kutoa maoni. Nasaba Bora anazaa mtoto na Lowella . Hata hivyo, Bi Zuhura anapomdadisi mumewe anamwambia mkewe asimwulize maswali mengi. Mwanamume wa Kiafrika aliye na mawazo sawa na ya Nasaba Bora ni sawa yanapofanywa na mwanamume bali ni hatia iwapo mwanamke atayatenda. Nasaba Bora anapomshuku mkewe kuwa si mwaminifu anampa talaka mara moja.Wake kama hawa wananyimwa haki za mapenzi nyumbani na mabwana zao. Nadharia ya ufeministi ina msimamo kuwa mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujikomboa na kujiondolea udhalimu anaotendewa na mwanamume.

Mwanamke anachukuliwa kama chombo cha kumnufaisha mwanamume kutokana na ndoa yake.Hii inadhihirika kupitia kwa mhusika Nana. Bw Hila anatuonyesha namna mwanamke alivyo na faida kwa jamii yake anapoolewa. Bwana Hila, ambaye ni babake Nana anasubiri apate gari, aina ya *Volvo* wakati Nana anapoolewa na mchumba ambaye amemchaguliwa**.** Tunaelezwa hivi: *"...Bado anazikumbuka zile nguvu za babake zilizomlazimisha yeye Nana kuolewa na mtu asiyemtunuku wala kumpenda .Eti kwa sababu ni tajiri ...*" (uk 159).Nana anaonekana kusumbuka kisaikolojia kutokana uamuzi wa baba yake kinyume na matarajio yake Nana. Hali kama hii inamdunisha mwanamke**.**

**3.2 Mauti**

Katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012), mamake Imani anakufa kwa sababu ya kupigwa na askari wa Mtemi Nasaba Bora. Imani anasononeka kwa uchungu kwa kumpoteza mamake mzazi. Mjane huyu anajikakamua kupigania haki zake kwa kukataa katakata

kuachilia shamba lake la Baraka. Kifo cha mjane huyu kinatendeka kutokana na ukatili wa Bwana Nasaba Bora Umebainika kuwa jamii nyingi za Afrika hawaheshimu wajane. Wengi wananyanganywa mali zao.Hii inadhihirika wakati mama yake Imani ananyanganywa shamba lake. Kifo cha mamake Amani kilikuwa pigo kubwa kwa jamaa hasa kwa Amani na nduguze. Watoto hawa wanapitia katika matatizo mengi. Mama angekuwa hai, angeonyesha mapenzi na familia yao haingesambaratita kama ilivyofanyika. Watoto hawa wangepata mahali pa kuegemea.

Ni wazi kwamba kifo cha mama yake Imani katu hubaki kama kumbukizi zenye uchungu kwa walioachwa bila tegemeo lolote kama inavyelezwa na Amani.

> *"...Ulikuwa wakati wa adhuhuri hivi, walipokuja askari na bastola mikononi …. Mama aliugua na kukata roho kutokana na kipigo alichopigwa. Oscar naye kaondoka. Alikoenda hakuna ajuaye … Mimi nikabaki peke yangu nilihisi huzuni na kupepea sana" (uk 58).*

Mtoto Uhuru Katika *Kidagaa Kimemwozea (2012)* anateseka chini ya ukatili wa Bwana Nasaba Bora. Mtoto huyu anapozaliwa na Lowela binti Maozi anatupwa mlangoni mwa mchungaji wake Amani. Ingawa alijua wazi asili ya mtoto Uhuru, hakutaka kumwauni.Chanzo cha kifo cha mtoto Uhuru ni dhiki anazokumbana nazo kutokana na ukatili wa Nasaba Bora. Maisha ya mtoto huyu yanazorota na mwishowe anaaga dunia kwa kukosa matibabu.

Bi Mkubwa Katika *Nyuso za Mwanamke ( 2010)* naye anapoolewa na Selemani anamwuua kwa kumpiga kisu na kuchoma nyumba yake. Bi Mkubwa anapopimwa na daktari anagunduliwa kuwa ni mgonjwa akilini kwa sababu ya hamaki nyingi. Baadaye anakufa kwa sababu ya ugonjwa wa akili (uk 387) .Yote haya yanaanza na udhalimu aliopata kutoka wanaume hao waliowahi kumwoa. Bi Mkubwa anateseka chini ya ukatili wa wanaume hawa. Anachoka kutokana na tabia mbovu ya wanaume hawa ambao wanamdhulumu. Hali inapozidi anaamua kuondoka, jambo ambalo limemsalimisha kutokana na kifo cha pole pole. Amegundua kwamba ni vigumu kwake kumpenda mtu asiyependeka.

### 3.3 Kukata tamaa kwa wanawake

Athari nyingine ya udhalimu dhidi ya wahusika wa kike ni kukata tamaa hasa pale ambapo mwanamke anapokabiliwa na matatizo asiyoweza kuyatatua. Nana katika *Nyuso za Mwanamke (2010)* anakata tamaa baada ya kuamua kuenda ambako anapata uhuru wa kibinafsi. Nana halitendi kitendo au kosa hili kwa kulipenda lakini kutokana na babake mzazi, Bw. Hila ambaye hangemruhusu apate uhuru wake. Nana anateseka kisaikolojia, jambo ambalo linakuwa nzito kwake, hayavumiliki na msichana mdogo kama yeye. Anaona dunia imefika mwisho, amekata tamaa. Anasema: "*Depression*" *nilimsikia -mpiga –gitaa kiwaaambia wanawake walionizunguka wakiashiria kujipata mabasi na tamaa...*'(Uk 62). Nana anaamua kwenda kuishi katika kijiji kingine.Akisema hivi:

> "*...Nimetoka nyumbani kwa hasira. Nikafutuka*
> *himaya ya babangu mzazi na mama wa kambo*

> *waliokuwa tayari siku zote kunirambisha asali kwa ncha za vidole iwapo ningefuata kanuni zao" (uk 135).*

Huu ndio uamuzi anauona bora baada ya kutosikilizana na babake. Msichana kulingana na utamaduni wa Kiafrika analelewa na kutunzwa vizuri ili baadaye atakapoolewa, wazazi wake waweze kuchuma kutokana na ndoa yake. Ili kuhakikisha kuwa hili limetendeka anachungwa ili asipotoshwe, na kuharibiwa na wanaume kabla ya ndoa. Baba yake Nana anamtatiza bintiye zaidi kisaikolojia. Hatimaye anakata tamaa na kutoroka kutoka kwao kwenda kuishi na wanawake wengine ambao wanapinga vikali udhalimu dhidi yao. Tunaelezwa hivi: *"... Aaaa, umekuja mwenzetu." Aligeuka Bi.Chuma na kuniona...Je,hapa ndipo mwisho wa safari? Niliondoka kwa kususia na hiyo njia ya kukimbia ukandamizaji ..." (uk 76.)*

Mwandishi anapomfanya Nana kutoroka kwao, anajaribu kumtafutia njia ya kumwauni na huo utamaduni unaomdhalilisha. Waandishi hawa waliandika kazi yao karne ya ishirini na moja. Wakati unavyozidi kuendelea, wanawake wanazidi kuzinduka. Wakati Bi Mkubwa ambaye ni mama yake Nana anapomwandikia barua, anamweleza kuwa utaja wakati wa bintiye ambao utakuwa tofauti na wao.

Hii ni kwa sababu watoto wa kike walipoendelea kupewa elimu ndipo wanazidi kupata kujua haki zao. Hali hii ilianza kulete mwamko mpya kwa watoto wa kike ambao walianza kuwa na sauti katika jamii. Ingawa mwanamke angali anadhulumiwa na tamaduni za kale, waandishi wanaonelea kuwa kuna mambo ambayo yanafaa kupigwa marufuku. Mojawapo ni ndoa za kulazimishwa, mahari

kuwekwa nyumbani kwa nia ya kumlinda mwanamke.Mielekeo hii wanaiona kuwa ni ya kionevu.

Kupitia kwa mhusika Nana inadhihirika vile inakuwa vigumu kwa msichana anayejua haki yake kuendelea kuvumilia udhalimu kutoka kwa wanaume. Nana anapoona ya kuwa hataweza kuufuata utamaduni unaomweka mwanamke katika nafasi ya pili, anaamua kuwa ataondoka katika kijiji alimokulia na kwenda katika kijiji kipya kuanza maisha ya ujamaa ambapo atashirikiana na wengine kujiendeleza.

Nana katika *Nyuso za Mwanamke* anachukua hatua na kuwaeleza wanajamii nia yake , ilhali Bi Zuhura na Bi Dora hawachukui hatua ya haraka kukataa kuendelea na kudhulumiwa.

Bi Mkubwa katika *Kidagaa Kimemwozea* anakata tamaa na kuondoka kwa Bw Hila. Aliondoka kutoka kwake kwa sababu ya maisha ya kufungiwa ndani . Bi Mkubwa anafanya uamuzi wa kumwuua bwanake.Tunalezwa hivi: *"...Alipoolewa na kufungiwa ndani, akili yake ilianza kufurugika mno mpaka ilimtuma kumsagia vigae mumewe na kumtilia ndani ya chakula kwa madhumuni ya kutaka kumwua..."* (uk 287). Hii inadhihirisha uamuzi ambao Bi Mkubwa anauona bora. Kumnyima mtu fursa ya kujieleza na uhuru anaoutaka kuna katiza tamaa na anayehusika kuamua kuchukua hatua nyingine.

Katika *Nyuso za Mwanamke (2010)* imedhihirika kuwa mwanamke wa Kiafrika anauwezo wa kujitegemea na kuweza kukataa udhalimu dhidi yake. Ameonyesha kuwa kujiepusha na udhalimu si jambo linalowezekana na kwa hivyo, mwanamke anaweza

kuishi vizuri bila ya kumtegemea mwanamume. Ukweli huu unajitokeza pale ambapo Nana, Bi Mkubwa, Bi Mau na Bi Chuma wanalazimika kuishi katika nyumba ya kupanga bila kutegemea wanaume. Hii inaonyesha wanajiondolea hisia za kujiona duni kutokana na vile walivyochukuliwa na wanaume zao.

Mwanamke anaonekana kuwa ndiye chanzo cha maovu ya jamii. Bi Mkubwa analaumiwa kuwa ndiye anayepinga jamii.Bi Mkubwa anasema hivi: *"... jamii yangu nzima ilikuwa dhidi yangu kila nilipotafuta uhuru wangu…" (uk* 285). Hii inadhihirisha kwamba jamii haimpi mwanamke nafasi yoyote ya kujieleza. Katika *Kidagaa Kimemwozea* Lowella anakata tamaa kwa kuacha masomo yake katika kidato cha tatu. Anapopata mimba anaifunga mkanda hadi akajifungua kitoto kilichotupwa mlangoni mwa Amani. Hata hivyo hii inatokana na udhalimu aliotendewa na Nasaba Bora wa kumtia mimba.

Bi Zuhura naye anakata tamaa baada ya kuishi katika ndoa iliyojaa mateso na ukatili wa bwanake Nasaba Bora. Anapewa talaka baada ya kushukiwa na Nasaba Bora kuwa alijihusisha kimapenzi na Amani. Tunaelezwa hivi: "...*Nyumbani kwa Mtemi Nasaba Bora,Bi Zuhura alipata talaka* ..." (uk 134) Hii inadhihirisha kuwa mwanamume anashiriki pakubwa katika kupoteza matumaini ya mwanamke, lakini jamii haimlaumu mwanaume ila mwanamke pekee. Vitendo anavyotendewa mwanamke na mwanamume kama vile kumhadaa kimapenzi ,kumpachika mimba na kisha kumkana ni ishara nzuri ya taasubi ya kiume.

### 3.4 Uhusiano wa unyumba

Athari nyingine ya udhalimu dhidi ya wahusika wa kike ni kuhusishwa kwenye ndoa ambazo daima dawamu hazina raha. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) Bi Zuhura anakiri kuwa "… *alikuwa na kiu lakini si ya maji… pia njaa lakini si ya chakula . Mwanamume habebeki kama mzigo wa moto* …"(uk 91) Kwake Bi Zuhura wanaume wangestahili wanawake wawaone kama abiria wenzao katika mashua ya maisha, dunia ingekuwa pahala pema zaidi pa kuishi. Ndoa kama hii huwa imepoteza ladha yake na huwa haiwafaidi wanandoa. Bi Zuhura anapoteza uhuru wa kutoa uamuzi wa mawazo. Mwanamke anapofanyiwa hivyo, inabainisha kukosekana raha katika ndoa yake. Bi Zuhura kama mhusika wa kike yupo tu katika ndoa kwa sababu ni lazima awepo.Bi Dora naye ameishi katika maisha magumu na yaliyojaa mateso kutoka kwa mumewe Majisifu Majirefu. Bi Dora ni hodari katika kazi za nyumbani na ulezi kwa watoto wasiojiweza. Bi Dora ameachiwa malezi ya watoto wanne na mumewe. Mumewe anapotaka kuwatupa majini watoto hawa anawatetea vikali. Bi Dora katika *Kidagaa Kimemwozea* anasema hivi: "...*likiwa bonge la nyama. Mtu hupata ajaaliwalo sio alitakalo*." (uk 31).

Katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) Bi Mkubwa anaishi maisha ya mateso na ukatili.Yeye Yeye ni mke wa kwanza wa Bw Hila na hapati uhuru aliohitaji.Pili anaolewa na Bw Simai ambaye kupigwa kulikuwa ni kama ada. Tatu anaolewa na Selemani kijogoo ambaye hatimaye Bi Mkubwa anaamua kumtoa uhai kwa kumdunga kisu. Haya yote yanamtatiza Bi Mkubwa kisaikolojia. Mwishowe anakuwa mwehu. Hii inadhihirisha kuwa bwana anachukuliwa kuwa mwenye mamlaka na kufanya uamuzi. Mtemi Nasaba Bora anazururazurura akikimbizana na kuwaharibu wasichana

wadogo na ila mke wake hana uhuru wa kumwuliza chochote. Wanaume kama hawa wanabaki wakiishi katika maisha ya kuwahuzunisha wanawake.

Nana na Bi Mkubwa katika *Nyuso za Mwanamke* (2010) wanachukua hatua ya haraka ili kujiondoa katika udhalimu huo. Umebainika kuwa mwanamke anafaa kuchukua hatua ya kuondoka katika jamii inayomdhulumu na kwenda kushirikiana na walio tayari kujiendeleza kwa madhumuni ya kujenga kizazi kipya kama afanyavyo mhusika Nana. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inahimiza ushirikiano ili kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

### 3.5 Upweke

Upweke ni hali ya kukaa katika maisha peke yako bila ya mshirika, mke au mume. Upweke unasababishwa na kukanwa na watu au jamii iliyokaribu na mhusika . Hata hivyo upweke huweza kusababishwa wakati mwanya umetokea kati ya mhusika na mhusishwa au wahusishwa. Pia vitendo vya kikatili vilivyoshuhudiwa na mtu inamfanya awe katika hali ya upweke kwa kuhofia kuwa chochote kinaweza kutokea kwa njia isiyomfurahisha. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) Bi Zuhura anaishi katika maisha ya ukiwa baada ya bwana yake kumdhulumu kimapenzi. Hali hii ya upweke inajidhihirisha wakati Bi Zuhura anaeleza kuwa mumewe anamazoea ya kuingia nyumbani usiku wa manane.Bi Zuhura anasema hivi: "*...Bi Zuhura alipojilaza katika kitanda chao chenye matendengu ya msonari na godoro lenye maki pana,alitafunwa na ukiwa na jakamoyo...*" (uk 90). Bi Zuhura anaishi katika hali ya upweke. Hali hii inasababisha kusumbuka kisaikolojia.Maswali mengi yanabubujika akilini mwa mhusika na mengi ya haya maswali hayana majibu.

Bi Dora naye anajipata katika upweke kutokana na mumewe ambaye ni mlevi na kusahau majukumu yake.Mara nyingi anatusiwa na mumewe eti alimzalia watoto walemavu na punguani ambao aliwaita mashata na masimbi.Bi Dora anadhalilishwa na mumewe na hakumthamini hata kidogo.Hii inamdhulumu Dora na hujipata akijisaga kwa kusema hivi:

> *"...Haya ni maisha gani?.Yalikeketa maini Dora. .Alijutia siku aliyokubali kufunga pingu za maisha na mwalimu Majisifu..".(uk 44).*

Bi Dora ni mwanamke mvumilivu mno .Analazimika kuvumilia ulevi na ugomvi wa mwalimu Majisifu. Dora anakubali yotei yaliyomfika na hapati usaidizi kutoka mumewe. Hali hii ya Dora inamfanya awe katika hali ya upweke.

Katika *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana anajipata katika hali ya upweke anapokosa upendo wa mama yake mzazi .Nana anasema kuwa*"...Mara tu baba alipompokonya mama haki ya kuwa mama na mimi bintiye.Haki ya kunikuza na kunilea kwa hisia na huruma..."(uk 61)* .

Bi Mkubwa katika*Nyuso za Mwanamke (2010)* naye ni mhusika anayeolewa na wanaume mara nne.Katika ndoa hizi zote hapati raha wala havumilii unyanyasaji wao. Bi Mkubwa analazimika kutoka katika ndoa zote nne. Anajikakamua na kuwaacha waume hao kwa sababu ndio njia ya pekee ambayo anaiona kuwa na nguvu ya kuweza kumkomboa. Tunaelezwa kuwa baada ya hapo Bi Mkubwa alipata taabu sana. Akaishi

maisha ya bahati nasibu.Alipopata kisabeho, cha mchana hakuwa na hakika nacho.Alipopata cha mchana chajio hakukitazamia.(uk 289).

Nana naye ni mfano wa mwanamke anayejisumbua kisaikolojia kutokana na upweke.Kinachomsumbua mwanamke huyu ni woga kutoka upande wa baba yake mzazi.Nana hapati yeyote anayeweza kumfariji ingawa anajipa moyo wa matumaini na kujiamini. Baadhi ya wanawake wengine katika riwaya hii wanaojipata katika upweke ni pamoja na Bi.Mkubwa Bi Mau na Bi Chuma.Umebainika kuwa hali hii ya upweke unasababishwa na kutengana na wapendwa wao.

**3.6 Woga**

Kulingana na Katola, E (2006) woga huletwa na vitisho vinavyotokana na watu wenye uwezo wa aina yoyote kuliko anayetishwa. Vitendo vya kikatili vinavyoshuhudiwa na mtu humfanya awe na woga kwa kuhofia kuwa vinaweza kutokea tena. Lowela katika *Kidagaa Kimemwozea* (2012) anapogundua kuwa ana mimba anaacha shule katika kidato cha tatu. Anapopata hiyo mimba anaifunga mkanda hadi kujifungua kitoto kilichotupwa mlangoni mwa Amani.

Lowela binti Maozi anaficha mimba kwa kuwa alifahamu kuwa kitendo kile siyo kizuri na ni kinyume cha maadili na matakwa ya familia yake na pia jamii kwa jumla.

Mtemi Nasaba Bora ambaye ni mhusika wa kosa hili hakabiliwi wala haishi kwa woga kama huu wa Lowela sababu yeye ni mwanamume . Hii imebaini kuwa mwanamume anayezurura ovyo ovyo na wanawake huchukuliwa kama “ dume” ilhali mwanamke ambaye anazururazurura ovyo ovyo na wanaume huchukuliwa kama amekosa maadili.

Hali kama hii inajitokeza kwa sababu jamii ya wahusika hawa ni ya mfumo wa kuumeni ambao huwapendelea sana wanaume na kuwadharau wanawake. Jamii haimlaumu mwanamume kwa sababu ya taasubi ya kiume inayojitokeza katika mfumo wa kuumeni. Nasaba Bora anajiona bora na anayefaa kuliko Bi Zuhura mke wake .Hii inabainika kuwa makaripio yake kwa Mkewe na uongo wa kuwa yuko kazini kusuluhisha migogoro ya shamba ilhali alikuwa anazururazurura ovyo ovyo inaonyesha kutawaliwa na kasumba za kiume kwani anajua kuwa hata yeye amekosea lakini jamii haitambui makosa hayo.

Mazungumzo kati ya Bi Zuhura na Nasaba Bora yamezorota na kilichobaki ni Nasaba Bora kumwamrisha na kumkaripia mkewe kila anapozungumza naye. Hali hii humfanya Bi Zuhura kumwogopa Nasaba Bora. Bi Zuhura ansema hivi: "... *Mtemi Nasaba Bora alikuwa mume mkali asiyesemeseka wala kuambilika, hasa na mwanamke mnyonge kama yeye...*" .Hali hii inamfanya Bi Zuhura kuingiwa na hofu. Katika *Nyuso za Mwanamke* (2010), Bi Mkubwa anaeleza jinsi alivyodhulumiwa na babake kwa kumwoza kwa lazima. Ananyimwa masomo yake ili apate kuolewa.(uk 290) Bi Mkubwa alitiwa hofu na babake anapomlazimisha kwa mwanaume ambaye hakumpenda yeye mwenyewe .Katika riwaya ya za *Nyuso Mwanamke* Bi Mkubwa anapoolewa na Selemani kijogoo anadhulumiwa sana. Bi Mkubwa anaishi kwa hofu kutokana na ukatili wa mume huyo.Tunaelezwa hivi:

> "....*Halikuwa rahisi kamwe...Mengi yamemkuta kwa uthubutu na ushupavu wake.Ametishwa kwa sheria.Ametishwa hata na kinyume cha*

*sheria...Ametishwa kuharibiwa ujanajike wake...”(uk189)*

Hii inadhihirisha kuwa wanawake wengi wanaishi maisha yaliyojaa woga kwani mara nyingi wanalaumiwa kwa makosa yasiyo yao.

## 3.7 Hitimisho

Katika sura hii, athari za udhalimu dhidi ya wahusika wa kike zimebainishwa. Inadhihirika kuwa udhalimu unaowakabili wahusika wa kike katika ndoa unakuwa ni kusambaratika kwa ndoa hizo. Kutokana na uchungu mwingi na maumivu ya kimwili na roho ndoa nyingi huishia kukosa ladha. Familia ambayo inahusisha wazazi na watoto wanashindwa kuishi pamoja kwa amani kutokana na kutoelewana na hatimaye kusababisha kutokuwa na raha kwa ndoa.

Utafiti wetu umeonyesha kwamba maisha ya mwanamke yanaharibika pale ambapo mwanamke anadhulumiwa na mwanamume hasa kupitia baadhi ya asasi za jamii . Imedhihirika vile vile kwamba baadhi ya wanawake wanakata tamaa katika maisha na kukataa kuishi kwenye aliko tena. Hii ni kwa sababu mwanamke anakosa matumaini katika ndoa iliyo na mateso. Shida zinawakabili mpaka wanaona kama hawawezi kupambana nazo wazisuluishe .Ukataji tamaa unawafanya wahusika wa kike kufanya uamuzi mkali kuhusu maisha yao,kama wafanyavyo wahusika wa kike katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke (2010)* na *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Riwaya hizi zinathibitisha mwelekeo wa Nadharia inayotumiwa katika utafiti huu kwamba mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujikomboa na bali si lazima kutegemea uamuzi wa mwanamume.

hata hivyo, inadhihirika kuwa wanawake wana matumaini iwapo wataungana na kupinga vikali udhalimu huo. Imebainika kuwa wanawake wa Kiafrika wanaweza kuwa mashujaa na kuweza kujikomboa na kuishi bila kudhulumiwa na mwanaume. Ukweli huu unajitokeza katika kipitia baadhi ya matendo yanatotekelezwa na wanawake wanaojitokeza katika kazi tulizozishughulikia.

# SURA YA NNE

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia matokeo ya utafiti huu kulingana na madhumuni yake na yale yanayodhihirika katika uchanganuzi wa vitabu vilivyoshughulikiwa. Pia katika sura hii kuna mapendekezo yanayokusudiwa utafiti wa baadaye katika kazi za fasihi.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatetea mwanamke wa Kiafrika anayekabiliwa na udhalimu kutokana na hali mbaya za kijamii zinazohalalishwa katika jamii. Asasi hizo ni kama vile ndoa ,dini na siasa . Pia inaonyesha kuwa nafasi ya mwanamke ni ya pili katika jamii nyingi za Kiafrika .

.

### 4.1 Matokeo

Katika utafiti wetu imebainika kuwa udhalimu dhidi ya mwanake ni suala linalojitokeza katika hali mbalimbali. Imedhihirika kwamba mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu na mwanamume ambaye anajiona bora na mwenye mamlaka kuliko mwanamke.Hali hii inamfanya amdharau mwanamke. Dharau zinajitokeza katika baadhi ya matamshi yanyotolewa kwa wanawake.Imebainika wazi kuwa wahusika wengi wa kike wanatusiwa. Matusi hayo yanamtia aibu na kuumiza nafsi ya mwanamke anayeelekezwa matusi hayo. Mfano wa matusi yanayotumiwa ni yale ya kumwita mwanamke jamvi la wanaume kama inavyodhihirika katika *Kidagaa Kimemwozea*. (uk 134) .

Kuwaweka wanawake katika nafasi ya pili baada ya wanaume kunasababishwa na taasubi ya kiume inayozidishwa na mfumo unaotokana na ugawaji wa majukumu na hivyo mwanaume kuwa na nguvu na mamlaka zaidi dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za kimaisha .

Imebainika pia kuwa wanawake wanapigwa na wanaume kama njia moja ya kuwaadhibu kwa sababu ya makosa wanayofanya ambayo huhusishwa na kumvunjia mwanamume heshima. Sababu kubwa hasa inayomfanya mwanamume kumpiga mwanamke ni kuwa mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu asiyeweza kuishi bila kumtegemea mwanamume. Mwanamke anatarajiwa ajinyenyekeze mbele ya mwanamume na kumtii.

Imebainika pia kuwa wanawake wanatawishwa . Wanawake wanatarajiwa kukaa nyumbani bila kutoka nje wasije wakakutana na wanaume wengine ambao si wa familia zao. Haya hufanyika kwa sababu mwanamke anachukuliwa kama kiumbe duni kilicho na udhaifu wa kimwili na kiakili. Tabia hii ya kuwatawisha wanawake imefungamanishwa na dini ya Kiislamu kwa madai kwamba maandiko ya Korani Tukufu , yanaipendekeza . Ni kutokana na maandiko haya ambapo mwanamume anajitwika mamlaka ya kiungu juu ya mwanamke. Wanawake hawapewi haki yao kikamilifu. Mwanamke haruhusiwi kutoa uamuzi wowote ule unaolenga jamii. Mwanamume ndiye anayeamua kila kitu hasa masuala yanayomhusu mwanamke moja kwa moja.

Imebainika kwamba watoto wa kike wanachukuliwa kama vitega uchumi kwani huozwa wanaume waliochaguliwa na wazazi. Katika ndoa hizi, mali hutolewa.

Kigezo kinachotumiwa katika kufanya ukaguzi kilikuwa utajiri na wala sio mapenzi. Mali inapolipwa wanaume wengi huanza kuona wake zao kama sehemu ya mali yao. Wanawake wanatumiwa na waume kama vyombo vya kujinufaisha. Utoaji wa mali ni suala ambalo limechukua mwelekeo tofauti. Kulingana na hapo awali mali ilitolewa kama ishara ya shukrani kwa wazazi wa msichana aliyeolewa. Ilieleweka kuwa paliachwa mwanya katika jamii ile kwani msaada wowote alioutoa katika jamii yake haukupatikana tena. Mali inatolewa kama zawadi wala sio njia ya kujipatia mali.

Kutokana na matokeo haya ni bayana kuwa madhumuni ya utafiti huu ya kuiainisha aina mbalimbali za udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kama ilivyojitokeza katika riwaya zilizoshughulikiwa yalitimizwa. Aidha madhumuni ya kueleza sababu zinazowafanya wanawake kudhulumiwa yalitimizwa. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inatetea mwanamke wa Kiafrika anayekabiliwa na udhalimu kutokana na hali mbaya za kijamii zinazohalalishwa katika jamii. Asasi hizo ni kama vile ndoa ,dini na siasa . Pia inaonyesha kuwa nafasi ya mwanamke ni ya pili katika jamii nyingi za Kiafrika .Matokeo yote ya kazi hii yanakubaliana na mwelekeo wa nadharia iliyotumiwa.

Imebainika kuwa baada ya wanawake wengi kushindwa kuvumilia mateso yanayosababishwa na wanaume, ndoa zinasambaratika. Haya ni baada ya mwanamke kugundua kuwa ndoa yenye doa haikaliki . Wengi wanaapa kutorudia tena waume zao huku wengine wakikubali kuwarudia waume wao baada ya waume kugundua makosa yao na kuyatubu. Mamlaka anayokabidhiwa mwanamume mara nyingi yanamfanya atumie vitisho ili kumwogofya na kumtia hofu mwanamke.

Tuligundua kuwa hatua zinazochukuliwa na wanawake wanaodhulumiwa zinaonyesha kwamba , mwanamke wa Kiafrika ametambua kwamba anadhulumiwa na anajaribu kupambana ili kuuondoa udhalimu unaomkabili. Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu inaheshimu uwezo wa mwanamke wa Kiafrika wa kujitegemea na inapuuza udhalimu dhidi yake.

Ilibainika kwamba ingawa wanawake wanajitahidi kupigania haki zao, wanakabiliwa na upinzani kutoka kwa wanawake wenzao ambao hawako tayari kuwapinga wanaume. Wanawake waliojitolea kupigania haki zao wamejitahidi kujikomboa na kuwakomboa wanawake wenzao wanaokandamizwa na wanaume ili jamii ya wanawake iweze kuishi bila udhalimu na uonevu kutoka kwa wanaume.

Imebainika kuwa taasisi mbalimbali kama vile utamaduni na ndoa zimechangia katika kumdhulumu mwanamke. Pia imedhihirika kuwa wanawake wanasawiriwa kama watu wa kutovumilia matatizo yanayowakumba na kuamua kuchukua hatua ya mara moja ili kujitenga na watesi wao.

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha wazi kwamba hali ya kimaumbile ya wanawake ndiyo inayowafanya wanaume kuwaona duni na dhaifu kuwaliko .Utamaduni wa Kiafrika pamoja na ndoa ni baadhi ya taasisi zinazotumiwa na mwanaume kumdhulumu mwanamke.

### 4.1.1 Mapendekezo

Tunapendekeza utafiti mwingine uchunguze suala hili katika tanzu zingine katika fasihi ya Kiswahili.

Wahakiki wajao wanahimizwa waliangalie suala la mwanamke kwa uzito zaidi hasa waonyeshe jinsi mwanamke anavyojikomboa na jinsi ambavyo usawa kati ya wanajamii unavyofikiwa ambapo mwanamke anahusishwa katika shughuli muhimu za kijamii.

Ni mapendekezo ya utafiti wa kazi hii kwamba utafiti wa baadaye uchunguze suala la udhalimu kwa wahusika wa kiume katika utanzu wa riwaya. Hii ni kwa sababu kuna haja ya kujua kama wanaume wanadhulumiwa na wanawake na ni hatua zipi wadhulumiwa wanazichukua kujinasua kutokana na dhuluma hizo.

Utafiti huu ni muhimu katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu umetoa mchango mkubwa katika kuziba pengo lililokuwepo la uhakiki wa udhalimu dhidi ya mhusika wa kike katika msingi wa nadharia ya Ufeministi.

# MAREJELEO


Adagala , K (1981) A *study of the Women Question and Imperialism in Kenya* .A seminar Paper.

Burhani , Z (1987) *Mwisho wa Kosa* .Nairobi: Longman Kenya .

Chesaina, C 1987) *Women in African Drama*. Tasnifu ya Ph.D . Chuo Kikuu cha Leeds.

De Beauvor , S (1949) *The Second Sex* . London: Pan Books Publishers.

Eagleton , M (1986) *Feminist Literary Criticism*. New York: Longman.

Freedman , E .B (2002) *No Turning Back*. New York.

Greer, G (1971) *The Female Eunuch* : New York.

Habwe , J (1995) *Maumbile si Huja* . Nairobi:J K F.

Katola , E (2006) *Usawiri wa Mhusika Wa Kike Katika Tamthilia za Kiswahili* . Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kathleen , N ( 1979) *The Sisterhood of Man* . New York.

Kezilahabi , E (1971) *Rosa Mistika* . Nairobi : Kenya Literature Bureau.

Lugano , R (1989) *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Martin, A (1975) *Women And Imperialism*. New York.

Mbatiah, M ( 2000) *Kamusi ya Fasihi* . Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing.

Mberia, K (1997) *Natala*.Nairobi: Marimba Publications.

Millet , K (1977) *Sexual Politics* .London. Virago Press.

Mohammed ,S.A(1980) *Utengano*.Nairobi: Longhorn Publishers

-------------(2000) *Kitumbua Kimeingia Mchanga*.Nairobi : Longman publishers.

------------(2010) *Nyuso za Mwanamke* .Nairobi: Longman Publishers.

Momanyi ,*C (1998) Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili* . Tasnifu ya *PhD*, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.(Haijajchapishwa).

-------------(2006) *Tumaini* , Nairobi : Vide~muwa Publishers.

Muindi , A (1990) *Usawiri wa Wahusika Makahaba katika vitabu* vya Said Ahmed Mohammed. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Mule, P. K (1991) *Swala la Wanawake katika Tamthilia ya Kiswahili* :Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ndungo, C.M (1985) *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.*Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Njogu , K .na Chimerah, R *(*1999*) Ufundishaji wa Fasihi : Nadharia na Mbinu.* Nairobi.JKF

Ogundipe –Leslie,*(*1984*) African Women ,Culture and Another Development* .The Journal of African Marxists.

Ramazanoglu *(*1989*) Feminism and Contradictions of Oppression.London.* New York.

Traore , S *(*2008*) Suala la Familia na Jamii katika riwaya sita za Said Ahmed.* Tasnifu ya Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Tuki: (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi:* Oxford University Press.

Steady,*F.C (*1981*) The Black Women Cross -Culturally.* Cambridge*:*Schenkam Publication.

Wafula, R .M (1999) *Uhakiki wa Tamthilia* . Nairobi: JKF.

Wafula, R.M na Kimani,N (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.Nairorbi.JKF.

Walibora ,K (2012) *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publication.

Wamitila, K.W (1999) *Nguvu ya Sala* . Nairobi :JKF.

---------------2003) *Kichocheo cha Fasihi* . Nairobi. Focus Publications Limited.

--------------(2003) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi* na *Vipengele vyake*.Nairobi Phoenix publishers.

----------------*(2008) Kanzi ya Fasihi : Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi Vide~muwa Publishers.

Wanyonyi, C.M (2011) Uhakiki wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na Said Ahmed:Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Wollstonecraft, M (1972*) A Vindiction of the Rights of Women.* Penguin Blackwell Publishers.